# Nipashe

Jumatano Julai 6, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580998 *

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

MWANGA WA JAMII

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,012,798,111/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Makamu** Mkuu wa Shule asimamishwa kazi kwa tuhuma mapenzi na mwanafunzi wake

UKURASA 7



**DYBALA AKARIBIA KUTUA INTER MILAN**

UKURASA 22



Catherine Mwakasege



Lucy Magashi

MATOKEO KIDATO VI:

# Shule mbili za kata zaangusha vigogo

• **Zote** ziko kijijini, wasichana bado hawashikiki, waliong'ara kitaifa waanika siri ya ufaulu... *Ukurasa 3*

## YALIYOMO



UKURASA WA 4

### MTUHUMIWA MAUAJI YA MWANAFUNZI AKAMATWA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia mtuhumiwa wa tukio la...

UKURASA WA 8

### CRDB YATUA DRC NA DOLA MILIONI 30 SOKONI

BENKI ya CRDB imekamilisha mipango ya kuzindua shughuli zake katika Jamhuri ya...

## Rais Samia abaini mabinti waliobakwa waugua fistula

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiwapongeza na kuwapa zawadi wanawake waliojifungua katika jengo jipya la Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya CCBRT, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



## 72 walivyonaswa operesheni Loliondo, wamo raia wa Kenya

UKURASA 2

**MICHEZO** MANARA AMWANGUKIA RAIS TFF UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mkuu wa Huduma Shirikishi wa Benki ya NMB, Nenyuata Mejooli (katikati), Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), Mercy Silla (kulia) na Makamu Mwenyekiti, Rose Romanus (kushoto), wakifurahi baada ya kuzindua Siku ya NMB iliyoadhimishwa na chama hicho, kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 72 wanaswa katika operesheni ya Loliondo, wamo raia Kenya

**Novatus Makunga,** ARUSHA

OPERESHENI maalum ya siku 10 iliyofanywa na Jeshi la Uhamiaji katika Tarafa za Sale na Loliondo wilayani Ngorongoro mkoani Arusha, imewanasa watu 72 walioingia na kuishi nchini kinyume cha sheria.

Jeshi hilo pia limefanya ukaguzi wa shughuli mbalimbali za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGO) yaliyoko katika tarafa hizo mbili.

Kwa mujibu wa Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji (ACI), Hosea Kagimbo, waliokamatwa ni raia wa Kenya 57, raia wa Ufaransa saba na walowezi wanane.

Kagimbo alisema kati ya watuhumiwa hao, 30 watafikishwa mahakamani huku 13 wakiachiwa huru ilhali wengine 29 uchunguzi bado unaendelea.

Hata hivyo, Kagimbo alisema zoezi hilo limekabiliwa na vikwazo vya baadhi ya watu kuyakimbia maboma yao na uchunguzi unaendelea wa kuwasaka.

Kamishina Msaidizi wa Uhamiaji huyo alieleza kuwa wamezifikia NGO 10 na walifanya mahojiano ya kina na wafanyakazi wake.

Kufanyika kwa operesheni hiyo kumetokana na agizo la Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, alipotembelea maeneo hayo Juni 15 mwaka huu wakati wa uwekaji wa alama za mipaka ya Pori Tengefu Loliondo.

Serikali imepunguza ukubwa wa Pori Tengefu la Loliondo kutoka kilometa za mraba 4,000 hadi kilometa za mraba 1,500 huku ikiacha kwa wananchi kilometa za mraba 2,500.

Pori hilo sasa linajulikana kama Pori Tengefu la Pololeti baada ya kupunguzwa ukubwa na kuwekwa kwa alama za mpaka. Pololeti ni jina la mto maarufu na muhimu uliopo ndani ya pori hilo.

# Rais Samia abaini waliobakwa wana fistula

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameonyesha kusikitishwa na taarifa kuwa miongoni mwa wagonjwa wanaopokelewa Hospitali ya CCBRT wenye tatizo la fistula ni watoto kuanzia umri wa miaka 11 hadi 12 kutokana na ukatili wa kubakwa.

Rais Samia aliambiwa hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akiteta na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa hospitali hiyo, Brenda Msangi, katika uzinduzi wa jengo la kutolea huduma ya afya ya uzazi, lililojengwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 44 (Sh. bilioni 101.2).

Kiasi hicho kinajumuisha gharama za ujenzi, vifaa na vifaa tiba pamoja na usimamizi ili kumpatia mwanamke huduma bora ya uzazi kuanzia ujauzito, kujifungua na uangalizi wa mama na mtoto.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, Rais Samia alisema, wakati akiteta na Mkurugenzi Mtendaji, alimweleza kuwa umri wa watoto kuanzia miaka 11 hadi 12 ni miongoni mwa wagonjwa wanaowapokea.

"Wana kesi wanazozipokea mtoto wa miaka 12 au 11 analetwa hapa akiwa na fistula na hii inatokana na watoto kubakwa, wale wanaotubakia watoto wanazalisha tatizo hilo, pia kuna vitoto vidogo kabisa miaka minne, mitano, sita wanapokelewa hapa wana tatizo la fistula.

"Ndugu zangu wana jamii tuone tatizo hili la ubakaji ambalo kwa kiasi kikubwa tunalifumbia macho kwenye jamii, hatulisemi hatuwapeleki kunakohusika kwenye vyombo vya sheria wale wanaokosea, matatizo makubwa wanawasababishia watoto wetu wanaowafanyia vibaya."

Alitaka kupunguzwa idadi ya wagonjwa wanaoishi na fistula Tanzania kwa kuepuka ndoa za utotoni, ubakaji na mimba za mapema.

"Kitoto kina miaka 12 kinapata ujauzito, kitoto miaka 13 kinakuja hapo hakiwezi chochote, amecheleweshwa nyumbani ameanza kusukuma mtoto anachana kila kitu, fistula hiyo tujitahidi kuacha mila ambazo zinaleta matatizo haya," alisema.

Akizungumzia taarifa alizozipata kutokana na manusura wa vifo vitokanavyo na uzazi baada ya kupata shida wakati wa kujifungua, alisema ndiyo wanaokwenda kama wagonjwa wa fistula na inakadiriwa Tanzania kuwa na wanawake kati ya 12,000 hadi 19,000 wanaoishi na tatizo hilo.

Kuhusu hospitali hiyo, alisema kwa siku inaweza kuhudumia wagonjwa wa nje wanawake 300 na ina jumla ya vitanda 140 na vinane vya kujifungulia.

**MUME KUSHUHUDIA MKE KUJIFUNGUA**

Rais Samia alisema ndani ya jengo hilo kuna vyumba vinane vinavyomruhusu mzazi kuingia na mwenza wake au ndugu yake wakati wa kujifungua.

"Hakuna wakati wa faraja kama wakati wa kujifungua ukiwa na mtu wako pembeni ambaye anakusaidia kukupooza, hii itasaidia sasa waume zetu kuona kishindo tunachopambana nacho mule ndani, itasaidia waone kinachotokea mule ndani.

"Kwa maana hiyo watasaidia kwenda kwenye uzazi wa mpangilio, watajitahidi kutoa huduma ya kutosha ili siku ikifika mama awe na njia nyepesi ya kumleta mtoto duniani. Mmenifurahisha naamini serikali wataiga mfano huu pia, lazima wale majamaa tuingie nao huko waone kinachoendelea."

Alisema, hajutii hospitali hiyo kuitwa jina la Samia Suluhu Hassan, kama alivyoombwa.

Alisema jengo hilo limeanza kutoa huduma tangu Januari 3, mwaka huu na hadi Juni 10, mwaka huu, jumla ya watoto 65 wamezaliwa, kati ya hao, familia tatu zilipata mapacha na wanawake wawili walikuwa wenye ulemavu ambao walitoka na hali nzuri.

Alisema wakati akitembelea hapo amekuta tatizo la uhaba wa watumishi na alimweleza Waziri Ummy zinazoweza kuzibika kwa haraka azishughulikie.

**AHUZUNISHWA TUKIO BUKOBA**

Rais Samia alisema takwimu za vifo vya watoto na wanawake wakati wa kujifungua zinaonyesha asilimia kubwa wanaofariki ni kutokana na upungufu kwa wanaotoa huduma.

"Ama upungufu wa weledi au dharau ya watoa huduma na usimamizi hafifu, hii inanikumbusha kesi iliyotokea juzi Bukoba wajawazito wawili walikwenda kupata huduma ya kujifungua hospitali, anaambiwa mlinzi waite manesi, mlinzi anasema 'nesi amesema nisifungue mlango'.

"Mwambie kuna kinamama wanataka kujifungua, 'nesi amesema nisifungue mlango' mpaka wakajifungulia getini kwa hivyo dharau hizi, uzembe huu, kutokuwa na usimamizi wa kutosha kunaleta maafa kwa wanawake wakati wa kujifungua.

"Ninadhani hatupaswi kupata hukumu hii, ingawa mwisho yakitokea tunasema Mungu ndivyo alivyoandika, kusingekuwa na uzembe Mungu asingeandika, waziri na watu wako msimamie hayo mambo kwenye vituo vya kutoa huduma."

**WAKUU MIKOA KUPIMWA**

Kuhusu lishe bora na huduma ya mama na mtoto, Rais Samia alimweleza Waziri wa Afya kuwa kuna haja ya kuingia tena mikataba na wakuu wa mikoa kulifufua na atakayeshindwa kufikia vigezo hafai kuwapo kwenye mkoa.

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu CCBRT, Brenda alimwahidi Rais kuwa watafanya kila linalowezekana waendelee kutoa huduma bora.

Waziri Ummy alimpongeza Mwenyekiti wa Bodi ya hospitali hiyo, Dk. Wilbroad Slaa kwa kuisimamia hospitali hiyo na Mkurugenzi ambaye sio daktari kitaaluma, lakini anafanya vizuri.

Mlezi wa hospitali hiyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliomba wadau wengine waunge mkono juhudi zilizofanywa kwa kupeleka fedha ili kuwasaidia Watanzania wanaofika kutibiwa.

Mwakilishi wa wadau wa maendeleo wa CCBRT, Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, alisema jengo hilo ni muhimu kwa sababu lina mchango mkubwa wa kukuza usawa wa kijinsia ambao Tanzania imefikia kiwango cha juu.

HABARI KITAIFA

# Serikali, kampuni wateta mradi uchimbaji graphite

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali ipo katika majadiliano na kampuni ya Uranex kwa ajili ya ujenzi wa mgodi wa madini ya bunyu (graphite) utakaoanza hivi karibuni.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika vijiji vya Namikulo, Namkatila na Matambarale katika Kata ya Chunyu wilayani Ruangwa mkoani Lindi.

Majaliwa aliwataka wananchi wa Wilaya ya Ruangwa wajiandae kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi zitokanazo na ujenzi wa mgodi huo.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amesema kila kwenye rasilimali kabla ya kuanza uwekezaji, lazima wahusika wajadiliane na serikali ili kubaini namna ambavyo itanufaika," alisema.

Alisema wakazi wa maeneo hayo watakuwa ndiyo wanufaika wa kwanza kutokana na shughuli mbalimbali zitakazoendelea kuanzia hatua ya ujenzi hadi uzalishaji.

"Kila shughuli itakayofanyika hapa ni fursa kwetu sisi wana-Namikulo na wana-Ruangwa kiujumla. Tujipange sawa sawa, serikali yenu ipo makini kuhakikisha mnanufaika na mradi huo," alisema.

Meneja wa Mradi wa Kampuni ya Uranex, Isaac Mamboleo, alisema kampuni yao inatarajia kuanza ujenzi wa mgodi huo katika mwaka huu wa fedha.

Alisema mradi huo ambao utahusisha vijiji saba, unatarajia kugharimu Sh. bilioni 625 na utazalisha ajira 950. Kati yake, 600 wakati wa ujenzi na ajira 350 wakati wa uzalishaji.

Mamboleo alisema kwa sasa wanakamilisha ujenzi wa nyumba 59 zenye gharama ya Sh. bilioni 3.6 kwa ajili ya kuwalipa fidia baadhi ya wananchi waliopisha ujenzi wa mradi huo.

Alisema baada ya kukamilisha ulipaji fedha kama fidia ya ardhi na mazao, pia wanajenga nyumba zenye ubora kwa ajili ya kuwafidia wananchi 59 waliokuwa na nyumba katika eneo la mradi.

"Nyumba hizo tunajenga nje ya eneo la mradi na kila mtu anajengewa nyumba kulingana na ukubwa wa nyumba yake ya awali," alibainisha.

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo wameziomba kampuni za uwekezaji zitoe kipaumbele kwa watu wanaoishi karibu na maeneo ya mradi na kwamba wamejipanga na wako tayari kwa kazi.

# ...Waliong'ara waanika siri

**Na Salome Kitomari**

WANAFUNZI walioongoza kitaifa kwenye somo la sayansi kwenye mtihani wa kidato cha sita wamefunguka ndoto zao na siri ya ushindi huo.

Wanafunzi hao ni kutoka Shule ya Sekondari ya St. Mary Mazinde ambao wote walithibitisha kuwa kumtanguliza Mungu, kusoma kwa pamoja, upendo na kufundisha wengine kumewasaidia kufikia malengo.

Mwanafunzi wa kwanza kwenye masomo ya sayansi, Catherine Mwakasege, alisema safari ya masomo siyo rahisi lakini walikuwa wanasali pamoja darasa zima na kufanya sala zake mwenyewe.

Alisema uongozi wa shule pia uliwasaidia kufikia malengo yao, kushirikiana na walimu na kwamba ushirikiano baina yao ulikuwa mkubwa kiasi kwamba walikuwa kama wanafamilia.

"Ninamshukuru Mungu sana, wapo wenye akili zaidi yangu wengi sana lakini mimi nimekuwa wa kwanza, niliamini nitaweza, sijawahi kuwa 10 bora au mwanafunzi bora darasa la saba wala kidato cha nne, lakini sasa nimekuwa," alitamka kwa tabasamu.

Alisema ndoto yake ni kuwa daktari bingwa wa moyo kwa sababu anaona watu wengi wanateseka kwa ugonjwa huo, wengine wakilazimika kupanda ndege kwenda nje ya nchi kusaka matibabu.

Mama wa Catherine, Lida Makundi, alisema amefurahi kwa kuwa mwanawe hakuwa na akili kuliko watoto wote Tanzania, akikumbusha kuwa wamemlea katika kumtegemea Mungu, bidii na usikivu.

# Shule za kata zaangusha vigogo matokeo kidato VI

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

BARAZA la Mitihani la Taifa (NECTA) limetangaza matokeo ya mtihani wa kidato cha sita mwaka huu, likibainisha wasichana kuendelea kung'ara kwa ufaulu katika masomo ya sayansi, huku shule mbili za kata zikiziangusha shule kongwe na zinazomilikiwa na taasisi pamoja na watu binafsi.

Akitangaza matokeo hayo kwa waandishi wa habari jana kwenye ofisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali huko Mazizini, Zanzibar, Kaimu Katibu Mtendaji wa NECTA, Athumani Amasi, alisema kuwa kati ya wanafunzi 10 bora wa masomo ya sayansi, saba ni wasichana kutoka Shule ya ST. Mary's Mazinde Juu ya mkoani Tanga na watatu ni wavulana kutoka Shule ya Tabora Boy's ya mkoani Tabora.

Alisema ufaulu wa jumla kwa mwaka huu umeongezeka na kufikia asilimia 99.97 ya watahiniwa wote 93,136 waliofaulu ikilinganishwa na mwaka jana ambao ni asilimia 99.06, sawa na wanafunzi 87,043.

Alisema kati ya watahiniwa hao, wasichana waliofaulu ni 40,907 (asilimia 99.51) na wavulana ni 52,229 sawa na asilimia 98.55.

Kaimu Katibu Mtendaji huyo alisema watahiniwa wa shule waliofaulu ni 84,404 (asilimia 99.87) ya waliofanya mtihani ambapo mwaka jana walikuwa 79,596 na watahiniwa wa kujitegemea mwaka huu ni 8,732 wakati mwaka jana walikuwa 7,447.

Kuhusu ubora wa ufaulu kwa madaraja, alisema watahiniwa wa shule 83,877 (asilimia 99.24) wamefaulu kwa daraja la kwanza hadi la tatu.

Alibainisha kuwa baraza limezuia matokeo ya watahiniwa 21 wa shule ambao walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mitihani kwa baadhi ya masomo na kupewa fursa ya kufanya mtihani mwakani 2023. Alisema baraza pia limefuta matokeo ya watahiniwa 15 waliobainika kufanya udanganyifu katika mitihani hiyo. Kati yao, 15 ni wa shule na wawili wa kujitegemea.

**SHULE ZA KATA**

Kiongozi huyo alizitaja shule 10 bora kitaifa, shule za serikali saba zikipenya, ingawa shule ya kwanza ni Kemebos ya Mkoa wa Kagera ambayo ni shule binafsi.

Kwenye orodha hiyo zimo shule mbili za kata; Ziba ya wilayani Igunga mkoani Tabora yenye mchepuo wa sanaa na Mkindi ya wilayani Kilindi mkoani Tanga iliyo na mchepuo wa sayansi, ikitoa wahitimu wa kidato cha sita kwa mara ya kwanza.

**SHULE 10 BORA**

Kemes (Kagera), Kisimiri (Arusha), Tabora Boys (Tabora), Tabora Girls (Tabora), Ahmes (Pwani), Dareda (Manyara), Nyaishozi (Kagera), Mzumbe (Morogoro), Mkindi (Tanga) na Ziba (Tabora).

**WATAHINIWA 10 BORA SAYANSI**

Catherine Mwakasege (St. Mary's - Tanga), Lucy Magashi (St. Mary's - Tanga), Muhewa Charles Kamando (Tabora Boys - Tabora), Minael Mgonja, Norah Kidjout, Jennifer Chuwa, Pauline Mabamba, Rachel Moshy (wote St. Mary's - Tanga), Kulwa Elias na Oscar Marabe (Tabora Boys - Tabora).

**WASICHANA 10 BORA SAYANSI**

Catherine Mwakasege, Lucy Magashi, Minael Mgonja, Norah Eliaza Kidjout, Jennifer Chuwa, Pauline Mabamba, Rachel Moshy, Dina Ngiga (wote St. Mary's-Tanga), Judith Benedictor, (Kilakala-Morogoro) na Julitha Silangwa wa Bright Future Girls (Dar es Salaam).

**WAVULANA 10 BORA SAYANSI**

Muhewa Kamando, Kulwa Elias, Oscar Marabe, Baraka Nyota, Don Mwakatoga, Pwali Njogela (wote Tabora Boys), Albert Mashauri (Mzumbe), Zafrullah Mohammed (Tabora Boys), Philipo Ngeleshi na Kennedy Mcharo (wote (Wari-Kilimanjaro).

**10 BORA LUGHA NA SANAA**

Hamza Ngosse (Songea Boys-Ruvuma), Charite Chonza (Zakia Meghji-Geita), Zilabhela Kombwey (Ksimiri-Arusha), Mebo Mgaya (Ahmes-Pwani), Gilead Gwaselya Tukuyu-Mbea), Albert Boniphace (Kisimiri), Abdallah Mtawanyika (Kemebos), Winifrida Sugoya (Ahmes), Hassan Buruhani (Musoma Mara) na Erick Mlay (Dareda).

**WASICHANA 10 BORA LUGHA NA SANAA**

Charite Chonza (Zakia Meghji), Zilabhela Kombwey (Kisimiri), Mebo Mgaya, Winifrida Sugoya (wote Ahmes), Grace Filemoni (Dareda), Nahya Ahmed (Zanzibar Commercial -Mjini Magharibi Unguja), Lisa Assey (St. Mary's Mzinde Juu - Tanga), Shaklina Mkandama na Mary Hiza (wote Ahmes) na Clementina Geay (Dareda).

**WAVULANA 10 BORA LUGHA NA SANAA**

Hamza Ngosse (Songea Boys), Gilead Gwaselya (Tukuyu), Albert Boniface na Vincent Temba (wote Kisimiri), Abdalla Mtawanyika (Kemebos), Hassan Burhan (Musoma), Erick Mlay, Innocent Elikunda, Elibariki Ammi na Abrahman Mussi (wote Dareda).

**WASICHANA 10 BORA BIASHARA**

Esther Chama (Kemebos), Dorcas Chacha (Arusha), Nasra Ali Omar (Zanzibar Commercial), Gladness Swai (Canossa -Dar), Gladys Amlima (Shabaaban Robert - Dar), Tecla Kilonda (Tusiime-Dar), Aisha Kilonda (Tambaza - Dar), Edna Urio (Weruweru - Kilimanjaro) na Esther Malebeto (Bukongo-Mwanza).

**WAVULANA 10 BORA BIASHARA**

Sultan Mohamed (Istiqama Islamic-Tanga), Yussuf Khamis (Tambaza), Denis Matemu (Sengerema-Mwanza), Mansury Mtandamo (Umbwe-Kilimanjaro), Richard Richard (Kemebos), William Maika (Rosmini-Tanga), Idrisa Ali Shaaban (Zanzibar Commercial), Ally Kondo (Baobab-Pwani), Bhizabhityo Bhizabhity na Waziri Angaluya (wote (Kibaha-Pwani).


BISMILLAH RAHMAN RAHIM



Familia ya marehemu **Dk. Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye Hitima ya kumuombea **Marehemu Dk. Omar Ali Juma** itakayofanyika siku ya Alhamisi tarehe **7 Julai, 2022 saa kumi jioni** katika **Msikiti Wa Ngazija**

Kufika kwenu ndio mafanikio yetu.

Ndugu, marafiki na jamaa wote mnakaribishwa.

**Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.**

**AMIN**

16928002

# Adaiwa kujinyonga kwa kutumia chandarua

**Na Neema Hussein,** MPANDA

JOYCE John (30) amekutwa amefariki dunia chumbani baada ya kudaiwa kujinyonga kwa kutumia chandarua huku chanzo kikiwa hakijafahamika.

Tukio hilo lilitokea jana katika Mtaa wa Misunkumilo, Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi ambako Joyce alikwenda kumuuguza mama yake mzazi.

Akizungumza na Nipashe jana, bibi wa marehemu, Elenee Stephano, alisema aliamka asubuhi kuelekea hospitalini kumwona mtoto wake ambaye ni mama mzazi wa Joyce na kumwacha mjukuu wake akiwa bado amelala na watoto wake.

Alisema baada ya kurudi nyumbani, alikuta mlango wa chumba alichokuwa amelala Joyce umefungwa kwa ndani huku mtoto mdogo wa marehemu mwenye umri wa miezi kumi akilia ndani, ndipo alipoanza kugonga mlango bila mafaniko.

"Niligonga sana mlango huku nikiita Joyce, nikigonga mtoto ananyamaza, nikitulia mtoto anaanza kulia, nikaingia chumbani nikawauliza watoto wengine wa marehemu, 'mama yenu yuko wapi?' wakasema hawajui," alisimulia bibi huyo.

Aliendelea kusimulia kuwa aliomba msaada kwa jirani ili kujua kilichokuwa kinaendelea ndani ya chumba hicho na baada ya kuchungulia dilishani, waliona mwili wa Joyce ukiwa unaning'inia juu ya 'kenchi' ndani ya chumba hicho.

Mume wa marehemu, Abel Daniel, alisema mke wake alimuaga anakwenda kwao kumuuguza mama yake mzazi na mara ya mwisho waliwasiliana juzi kutaka kujua hali ya mgonjwa.

Abel alisema alipigiwa simu akiwa kazini akitakiwa arudi nyumbani kuna tatizo na akipiga simu ya mke wake inakatwa na kwamba alipofika nyumbani, alikuta watu wamejaa nyumbani kwa mama mkwe wake.

"Mimi baada ya kufika hapa kuona watu wamejaa nikajua mama mkwe kafariki dunia kwa sababu ndiye aliyekuwa mgonjwa kumbe mke wangu! Hata sijui nini kimemkuta, ni bora angeacha hata ujumbe tujue tatizo nini limemfanya achukue uamuzi huo," alisema.

Baadhi ya majirani wa mtaa huo, walidai walisikia kelele za watu wakilia, wakajua mama mzazi wa Joyce amefariki dunia lakini baada ya kufika eneo la tukio, wakakuta Joyce amejinyonga.

Akizungumzia tukio hilo, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa, Maria Joseph, alisema alipata taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa na baada ya kufika katika nyumba hiyo, aliushuhudia ukweli huo.

Askari polisi walifika kwenye eneo la tukio na kuuchukua mwili wa Joyce kwa ajili ya uchunguzi.




Meneja Mauzo wa bidhaa za Intanet Tigo, Edwin Mgoa, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa utambulisho simu janja kutoka Xiaomi na Red mi note 11, katika maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Barabara ya Kilwa Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja Mauzo wa Xiaomi Tanzania, Alex Katagira **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtuhumiwa mauaji ya mwanafunzi akamatwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia mtuhumiwa wa tukio la mauaji ya Rachel Michael (7) lililotokea mwishoni mwa mwezi Mei, mwaka huu, Misugusugu.

Katika tukio hilo, mtuhumiwa huyo anadaiwa kumnajisi mtoto huyo na baadaye kumuua na kisha kutoroka.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Gregory Mushi, alithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo na kwamba hatua za kisheria zinaendelea.

Katika tuko lingine Kamanda Mushi alisema mtu mmoja amekamatwa kwa tuhuma za kumtorosha mfanyakazi wa ndani anayedaiwa kumjeruhi mtoto wa miaka mitano kwa kumwagia mafuta ya moto.

Mushi alisema mwanafunzi huyo wa chekechea alimwagiwa mafuta ya moto juzi majira ya saa 11 asubuhi na mtuhumiwa aliyefahamika kwa jina moja la Rehema (14-15), mkazi wa Mbwewena ambaye alikuwa mfanyakazi wa ndani.

Alisema mtoto huyo alijeruhiwa usoni na mkono wa kulia.

Kamanda Mushi alisema baba mzazi wa mtoto huyo amekamatwa akidaiwa kumtorosha mtuhumiwa huyo.

# Jaji Mkuu atoa neno mawakili wa Zanzibar

**Na Grace Gurisha**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amesema mawakili wa Zanzibar kuja kufanya kazi Bara sio jambo baya, bali ni njia mojawapo ya kuwajengea uwezo kwakuwa watakutana na changamoto mbalimbali za kisheria zitakazowafanya wawe wazuri zaidi.

Profesa Juma alieleza hayo jana, baada ya Jaji Mbarouk Salim Mbarouk, kuomba ufafanuzi wa jambo hilo ambalo huulizwa na wanafunzi wa sheria na wadau wa sheria, wakati akizungumza na Baraza la Skuli ya Sheria Zanzibar ofisini kwake, Dar es Salaam.

Akijibu ombi hilo, Profesa Juma alisema atazungumza na Baraza la Sheria nchini kuona mawakili na wahitimu wa Shule ya Sheria Zanzibar kuja kufanyakazi za Sheria Tanzania Bara.

"Mawakili wa Zanzibar kuja kufanya kazi bara ni jambo zuri kwa sababu ni njia mojawapo ya kuwajengea uwezo kwa kuwa watakutana na changamoto mbalimbali za kisheria ambazo zitawafanya wawe wazuri zaidi," alisema Profesa Juma.

Alisema maombi yote ameyapokea likiwamo suala la mawakili na wanasheria wa Zanzibar kuja kufanya kazi Bara sio tatizo, kama mawakili wa nje ya nchi wanaruhusiwa hakuna uzito, atakaa na wenzake na baraza la sheria nchini kuliangalia suala hilo.

Katika mazungumzo hayo, Profesa Juma, aliuomba pia uongozi wa shule hiyo ya sheria kuwajenga uwezo wanafunzi wa shule hiyo kwa kuwapa mafunzo ya ziada nje ya taaluma yao, ikiwamo masomo ya biashara ili wakikosa kazi wawe na cha kufanya.

Pia aliwataka wawejengee uwezo katika masuala ya Sayansi na Teknolojia kwa kuwa hali ya ajira kwa sasa sio nzuri na hata ikiwezekana wafate ujuzi nje ya nchi.

Jaji Mbarouk ambaye ni Mwenyekiti wa baraza hilo, alisema wanafunzi na wadau hao huwauliza namna skuli hiyo itashauriana na uongozi wa Mahakama ya Tanzania kuona uwezekano wa kuwawezesha wanafunzi wanaomaliza Skuli ya Zanzibar kufanya kazi ya Sheria Tanzania Bara.

Alisema hivi sasa lipo sharti la sheria kwamba wakili kutoka nje ya Tanzania Bara, lazima awe amefanya kazi miaka mitano kabla ya kuruhusiwa kufanya kazi humo, na kwamba sharti hilo linawavunja moyo wanafunzi waliopo skuli ya sheria.

HABARI KITAIFA

# Mwanafunzi afungua kesi akitaka umri miaka 18 kugombea ubunge

Na Grace Gurisha

MWANAFUNZI wa Shule ya Sheria Tanzania (Law School of Tanzania), Alphonce Lusako, amefungua kesi Mahakama Kuu ya Tanzania akiomba itamke kwamba raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 ana haki ya kugombea ubunge.

Lusako amefungua kesi hiyo, namba 6/2022 dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), akidai kwamba Ibara ya 67(1) inakinzana na ibara nyingine za Katiba ya Tanzania kinachokataza vijana wenye umri kati ya miaka 18 hadi 21 kuchaguliwa kuwa wawakilishi katika Bunge huku Sheria za uchaguzi zikitoa haki moja ya kupiga kura kwa vijana hao.

Alidai, kifungu cha 67(1) cha Katiba kinasema; 'bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge endapo (a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano aliyetimiza umri wa miaka 21 na ambaye anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza'.

"Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Uchaguzi Tanzania kinasema; ili raia wa Tanzania asajiliwe na awe na sifa ya kupiga kura, ni sharti awe na umri wa miaka 18 au wakati wa kupiga kura atakuwa amefikisha umri wa miaka 18," alidai Lusako.

Alidai vifungu hivyo vinakinzana na katiba inayosisitiza misingi ya demokrasia, uhuru na haki ya kijamii, usawa wa raia wote bila ubaguzi wa aina yoyote.

Alidai kifungu cha 13(1)(2)(5) cha Katiba kimefafanua juu ya haki sawa na usawa mbele ya sheria bila kuweka masharti ambayo kwa taathira yake ni ya kibaguzi.

"Kifungu cha 21(1) cha Katiba kinatoa haki ya uhuru wa raia kushiriki shughuli za umma wakati kifungu cha 29(1) cha katiba kinatoa; haki ya kufaidi haki za msingi za binadamu, na matokeo ya kila mtu kutekeleza wajibu wake kwa jamii, kama zilivyofafanuliwa katika ibara ya 12 hadi 28 ya katiba," alidai.

Alidai mtu anapofikia umri wa miaka 18 anachukuliwa ni mtu mzima na sheria imeweka nadharia kwamba anaweza kufanya maamuzi sahihi kwa kuwa anakuwa amekomaa kiakili na ndiyo msingi wa Sheria za uchaguzi kutoa haki kwa vijana kati ya miaka 18-21 kupiga kura.

Pia alidai kuwa hakuna hoja za kitafiti zinazoweza kuthibitika kwamba kijana mweye umri wa miaka kati ya 18 na 21 hana utashi na hivyo kukosa haki ya kugombea ubunge na kama ndivyo, waliopaswa kupiga kura walipaswa kuwa watu wenye umri wa miaka 21 na sio wenye umri wa miaka 18.

Mwanafunzi huyo, pia anaiomba mahakama hiyo imwamuru Mwanasheria Mkuu ndani ya mwezi mmoja baada ya hukumu hiyo awasilishe kwa Msajili wa Mahakama Kuu na kwake maelezo ya mwongozo wa hatua zilizochukuliwa kutekeleza hukumu hiyo ambao utakuwa sehemu ya kumbukumbu za mahakama.

Pia, anaiomba mahakama hiyo imwamuru Mwanasheria Mkuu katika kipindi cha miezi mitatu baada ya hukumu aandae na kuwasilishwa kwa wadau muswada wa mapendekezo ya marekebisho ya kikatiba katika kutekeleza amri ya mahakama.

# Matatani tuhuma kutoa taarifa za uongo kortini

Na Grace Gurisha

DALALI wa Mahakama, Charles Sengo na mfanyabiashara, Shabani Kobla wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, wakikabiliwa na mashitaka 31 yakiwamo ya kutoa taarifa za uongo mahakamani.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Suzan Kihawa, Wakili wa Serikali, Kija Elias, alidai kuwa Machi 23, 2012 mtuhumiwa Kobla alitoa taarifa za uongo.

Ilidaiwa kuwa taarifa hiyo aliitoa katika kesi ya madai namba 99 ya mwaka 2012, akionesha kwamba Escan Berewell Co Ltd ni kampuni iliyosajiliwa Tanzania wakati akijua sio kweli.

Alidai kuwa Aprili 11, mwaka 2019, katika Mahakama ya Kisutu, Dar es Salaam, ilidaiwa kwamba mshtakiwa huyo akiwa mshindi, mmiliki na Mkurugenzi wa Kampuni ya Fahak Investment Ltd, kwa udanganyifu alijipatia Sh. milioni 185.

Elias alidai mshtakiwa alijipatia fedha hizo zilizokuwa katika akaunti ya mahakama katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na kuingizwa katika akaunti ya Fahak Investment Ltd, fedha ambazo zilitokana na mnada wa hadhara uliofanyika Septemba 11, 2016 kama ilivyoamriwa katika shauri la mwenendo wa utekelezaji wa hukumu.

Ilidaiwa pia Kobla alijipatia magari matatu aina Ashock Lyland kwa njia ya udanganyifu kwa madai kwamba yaliuzwa katika mnada wa hadhara.

Elias alidai, Juni 20,2016 mshtakiwa Sengo alitoa taarifa za uongo mahakamani hapo akionesha kwamba alimuuzia Mariamu Hamadi, magari matatu aina ya Layland Ashock kwa nyakati tofauti ambayo yote yana thamani ya Sh. milioni 200.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 26 ya kutoa taarifa za uongo kwa mtumishi wa umma, matatu ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na mawili ya kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu.

Upande wa mashtaka ulidai, upalelezi umekamilika na kuomba tarehe ya kuwasomea washtakiwa hoja za awali na hakimu alipanga Julai 6, mwaka huu.

Washtakiwa wote walipelekwa mahabusu kwa kushindwa kutimiza masharti ya dhamana, ikiwamo kuwasilisha mahakamani nusu ya fedha wanazodaiwa kujipatia kwa njia ya udanganyifu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI

TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'

1. UTANGULIZI:
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe na Kozi ya lami kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Kampasi ya ICoT - Mbeya na ICoT – Morogoro kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalumu ya vikundi vya Wanawake na Vijana ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | Wiki Nne (4) 08/08/2022 – 03/09/2022 | Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya) |
| 2 | Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | Wiki Nne (4) 12/09/2022 - 08/10/2022 | Mkoani Morogoro (ICoT – Morogoro) |

2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:

(a) Kozi Maalumu ya vikundi vya Wanawake na Vijana ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:

Kozi hii, Washiriki watajifunza maada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni kwa vikundi, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege. Kipekee, kozi hii imelenga kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

(b) Kozi ya Lami (Surface Dressing for low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:

Kozi hii, Washiriki watajifunza mada mbalimbali juu ya ujenzi wa barabara za lami (Surface Dressing for low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni: Maada juu ya vifaa na Mitambo midogomidogo, Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na matengenezo ya barabara za lami.

3. NJIA ZA UFUNDISHAJI
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

4. MALENGO YA KOZI
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:
i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

5. WALENGWA WA MAFUNZO:
a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

6. LUGHA YA MAFUNZO:
Lugha itakayo tumika katika Kozi ya Lami kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo itaendeshwa kwa muda wa wiki nne (4) ni Kiingereza; kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

7. ADA ZA USHIRIKI
a) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads)
i. Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,000,000.00

b) Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana
i. Mshiriki atakaye jitegemea huduma za chakula na malazi, atalipa ada kiasi cha Tsh. 350,000; na
ii. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 500,000.00

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

WASILIANA NASI
MKUU WA CHUO

TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,

S.L.P 963,
MOROGORO.
Simu : 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net

S.L.P 1957,
MBEYA.
Simu : 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com

216932902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko Sheria ya Ndoa hayakwepeki

**JANA** Rais Samia Suluhu Hassan, alisema miongoni mwa kesi zinazopokelewa Hospitali ya CCBRT jijini Dar es Salaam, ni watoto wenye umri mdogo wa miaka 11 na 12 wakiwa na fistula na miongoni mwa sababu ni ubakaji.

Rais alikuwa akizindua majengo ya kutolea huduma ya afya ya uzazi hospitalini hapo.

Wakati akiteta na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa hospitali hiyo, Brenda Msangi, alimweleza kuwa wagonjwa wanaopokelewa miongoni mwao ni watoto.

Watoto kati ya miaka 12 au 11, hupokelewa wakiwa na fistula baada ya kubakwa, wanaofanya hivyo wanazalisha tatizo la maradhi. Kiongozi huyo alisikitishwa jamii kufumbia macho tatizo la ubakaji kwa kutolisema na wanaotenda hawafikishwi kwenye vyombo vya sheria.

Alipotembelea wodini aliona mtoto wa miaka 12 na 13 ana ujauzito, ambaye hajui kitu kiasi cha kupata maradhi wakati wa kujifungua na wajawazito 12,000 hadi 19,000 wanaishi kwa tatizo hilo.

Alichokisema Rais ni tatizo halisi kwenye jamii kwa ambao wamejitokeza kufuata huduma za afya, lakini wapo waliofanyiwa ukatili kwa kulazimishwa kuolewa au kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wao kwa kuwa sheria inaruhusu.

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inaruhusu mtoto wa kuanzia miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi au walezi wake, huku Katiba ya nchi ikitambua umri wa miaka 18 kama mtu mzima.

Mwanzoni mwa mwaka 2016, Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, kupitia wakili Jebra Kambole, walifungua kesi kupinga kifungu cha 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa kinachoruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 kwa kibali cha mahakama na ridhaa ya wazazi.

Aidha, Julai 8, mwaka 2016, Mahakama Kuu ilitoa hukumu ikikubali kwamba vifungu hivyo vya sheria ya ndoa vinapingana na Katiba ya nchi kwa kuweka umri tofauti wa kuoa na kuolewa kati ya mtoto wa kike na kiume.

Aidha, serikali ilisema inaangalia uwezekano wa kufanyia marekebisho Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, kwa kushirikisha wadau wote muhimu.

Tunaungana na wanaharakati na wadau wengine juu ya umuhimu kwa kufanya marekebisho ya sheria hiyo, ili kuwaokoa watoto wa kike dhidi ya adha wanazopitia.

Katika umri wa miaka 14 bado viungo vya uzazi havijamudu mikikimikiki ya kubeba mimba na kulea mtoto, bali wanapaswa kuendelea kimasomo kwa nyanja mbalimbali.

Kutokana na sheria hiyo watoto wanakosa haki ya kusoma kwa baadhi ya jamii ambazo zinawaozesha wakiwa wadogo kwa kisingizio kuwa wamekubali, lakini kimsingi hawajakubali tamaa ya kupata mali.


Wengine wanaoolewa lakini bado hawajaweza kumudu mahitaji ya ndoa na kuhudumia familia, kwa kuwa ni jambo lenye kuhitaji mtu aliyekomaa kiakili.

Ni muhimu serikali ikaharakisha mchakato ili kuunga mkono jitihada za wadau ambao wanafanyakazi na jamii ngazi ya chini na wanaona tatizo lilivyo kubwa.

Kwa alichokishuhudia Rais jana ni jibu tosha kwamba kwenye jamii kuna tatizo kubwa ambalo linahitaji kushughulikiwa, ili kuwaokoa watoto wa kike wafikie ndoto zao.

Kuacha sheria hiyo kuendelea kutumika ni kichaka cha watu kuendelea kuwaumiza watoto wa kike kwa kuwalazimisha kuolewa na kuwaathiri kisaikolojia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ukomavu wa kisiasa unaweza kumaliza migogoro ya vyama

**NDANI** ya vyama vya siasa kumekuwapo na mvutano unaochangiwa na sababu mbalimbali, ikiwamo kutofautiana hoja, mawazo, mitazamo na maoni miongoni mwa wanachama au na viongozi wao.

Mazingira hayo husababisha wengine kuhama vyama, kufukuzwa au kuendelea kubaki huku wakisuguana na kuvifanya visipige hatua mbele kutokana na migogoro.

Wapo ambao hukutwa na hatia na kupewa adhabu kama kufukuzwa au kutakiwa kuomba radhi ili maisha yaendelee, lakini badala yake wanabaki kuendeleza migogoro ambayo haina afya kwa taasisi zao.

Kwanza migongano au migogoro katika vyama haliepukiki, kwa sababu vinakutanisha watu tofauti na wenye mtazamo inayotofautiana, hivyo jambo la muhimu ni ukomavu na kisiasa.

Ninaamini kukaa na kujadiliana mambo yao na kupata muafaka suala ambalo linaonekana haliendi sawa ni muhimu kwa ustawi wa chama cha siasa.

Hivyo, hali ikishafikia kumfuta mtu uanachama, kama ana mapenzi na chama, kinachofuata ni kuomba radhi ili arudishwe kundini ili kuendelea kukitumikia badala ya kukumbatia migogoro inayoweza kusambaratisha chama.

Kimsingi, ni wazi kwamba kwenye suala la kuomba radhi, wapo baadhi ambao wamejaliwa busara na hufikia kuomba hata kama hawajafanya kosa, lengo likiwa ni kuepusha malumbano yasiyo na msingi.

Hivyo, ni vyema kama wanasiasa wangekuwa na utamaduni huo kwa kutafakari na kisha kuchukua hatua ambazo zitasaidia kuzima migogoro ndani ya vyama vyao ambayo inaweza kusababisha wananchi wasiviamini.

Ninaamini kwamba kuomba radhi ni hatua moja na kusamehewa ni jambo muhimu, hasa kwa kutambua kuwa hakuna binadamu aliyekamilika, hivyo kukaa na kumaliza tofauti ni bora.

Chama ni wanachama na bila wanachama hakuna chama, hivyo kuwapo kwa migogoro na kisha kufukuzana, sidhani kama ni jambo jema, na si vizuri wanachama kufurahia pale mwenzao anapofukuzwa.

Ndiyo, inawezekana kada akawa amekwenda kinyume na taratibu za chama na kufutiwa uanachama, ni sawa, lakini ingefaa hatua hiyo ikachukuliwa kwa umakini wa hali ya juu, ili kuepusha migogoro.

Ni kweli kwamba, migogoro ni sehemu ya maisha ya kila siku ya mwanadamu, kwani hutokea kwa sababu kila mmoja ana mahitaji, na kwa bahati mbaya rasilimali za kutimiza mahitaji hayo hazitoshi.

Licha ya kutotosha kwa rasilimali, lakini namna ya kufikia mahitaji hayo hakuingiliani au hakufungamani kati ya mtu na mtu au kundi na kundi. Kutoingiliana ama kutofungamana kwa namna ya kuyafikia mahitaji husababisha kutokea kwa migogoro.

Lakini baadhi ya migogoro ni midogo inaweza kusuluhishwa, mingine ni mikubwa kiasi kwamba huacha madhara makubwa yasiyoweza kurekebishwa au huchukua muda mrefu kupona.

Wadau wa siasa walishawahi kuelezea kuwa vyanzo vya migogoro ya ndani ya vyama hivyo, ni upendeleo kwa baadhi ya wanachama na kuwatenga wengine, kukosekana kwa mgawanyo sawa wa rasilimali ambapo kiongozi wa chama hupata mgao mkubwa kuliko wengine.

Kwamba, kukosekana kwa mgawanyo mzuri wa rasilimali na mamlaka kuegemea upande wa juu tu husababisha tatizo la kiuongozi ambalo huzaa migogoro inayoweza kusambaratisha vyama.

Kukosa ajenda za msingi kwa vyama vya siasa ambapo huweza kusababisha kutokea kwa migogoro, hasa panapotokea baadhi ya wanachama kutaka ajenda maalumu ambayo chama itakibeba kama msingi wa kujitofautisha na vyama vingine na kuandaa sera mbadala ya kuiuza kwa umma.

Vilevile kuna suala la imani, itikadi, falsafa na uvumilivu dhidi ya mabadiliko, ambapo vinasababisha wale ambao hawataki kubadilika kujikuta wakizua migogoro kati yao na viongozi wao bila sababu za msingi.

Lakini pamoja na yote hayo, ukomavu wa kisiasa ni nguzo muhimu ndani ya vyama ambayo viongozi wanaweza kuionyesha na kuitumia kumaliza migogoro katika vyama vyao.

# Ajali ilivyoua watano

**Na Waandishi Wetu,** MBEYA

WATU watano wamefariki dunia na wengine ambao idadi yao bado haijafahamika kujeruhiwa baada ya lori la mizigo lililokuwa limesheheni magunia ya mahindi likitokea mkoani Songwe kuelekea Dar es Salaam, kufeli breki na kuligonga basi dogo la abiria aina ya Toyota Coaster.

Ajali hiyo ilitokea jana jioni katika eneo la Inyala Relini, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, eneo hilo likisifika kwa kuwa na mkusanyiko wa watu wengi.

Mbali na ajali hiyo kusababisha vifo na majeruhi, pia ilisababisha uharibifu wa miundombinu ya umeme kwa kuangusha nguzo na kukata nyaya za umeme.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alilitaja lori hilo kuwa ni lenye namba za Usajili T 317 DWL na Tela namba T 804 BMF ambalo lililigonga basi lenye namba za usajili T 201 DUN.

Kamanda Matei alisema kuwa baada ya lori hilo kuligonga basi hilo, lililiburuza mpaka kwenye makazi ya watu umbali wa zaidi ya mita 100 kutoka eneo la ajali na kwamba dereva wa lori hilo bado hajulikani aliko.

Alisema mbali na kuligonga basi hilo, lori hilo pia liligonga vibanda vya wajasiriamali wanaofanya shughuli zao pembezoni mwa barabara hiyo ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

"Idadi ya majeruhi bado hatujaipata lakini nikitoka hapa ninaelekea hospitalini kwa ajili ya kufuatilia idadi yao na hali zao, maana taarifa za awali ni kwamba wengi wao wameumia sana," alisema Kamanda Matei.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo walisema chanzo cha ajali hiyo ni barabara hiyo kuwa nyembamba, hivyo magari yanashindwa kupishana, hasa kunapotokea dharura.

Mmoja wa mashuhuda hao, Mathias Kapesa, alisema wakati ajali hiyo inatokea, alikuwapo eneo la tukio na alishuhudia wakati lori hilo linaanza kuligonga gari dogo mpaka lilipovamia vibanda na kwenda kuvamia nyumba moja iliyoko pembeni.

"Tunaomba serikali iipanue barabara hii maana hapa ni nyembamba mno na ikiwezekana watutenganishie magari makubwa na madogo ili kuepusha madhara kama haya ambayo yametokea hapa," alisema Kapesa.

Yunga Mwandemele alisema ajali hiyo ni ya tatu kutokea katika kipindi cha wiki moja na hivyo akaiomba serikali kuiboresha barabara hiyo.

***Imeandaliwa na Nebart Msokwa na Grace Mwakalinga**

# M/Mkuu asimamishwa kazi tuhuma kujihusisha mapenzi na mwanafunzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAKAMU Mkuu wa Shule ya Sekondari Singida, Manispaa ya Singida, Thomas Ngiracha, amesimamishwa kazi kwa muda usiojulikana kwa tuhuma za kujihusisha kimapenzi na mwanafunzi wa kidato cha nne (jina tunalihifadhi) wa shule hiyo.

Mkuu wa Shule hiyo, Joseph Shani na Mkurugenzi wa Shule, Matliga Makuza walithibitisha kuchukuliwa kwa hatua hiyo dhidi ya mwalimu huyo.

Mwalimu Ngiracha (mtuhumiwa) alipoulizwa kwa njia ya simu alikiri kusimamishwa kazi kutokana na kuhusishwa na tuhuma hizo na kwamba suala hilo linashughulikiwa na vyombo vingine vya sheria.

"Ni kweli suala la kunihusisha mimi na tukio hilo zipo, lakini kimsingi sio za kweli, kwa sasa linashughulikiwa na vyombo vingine vya sheria," alisema.

Naye, Mkuu wa Shule huyo, Shani akizungumza na gazeti hili ofisini kwake alisema mwalimu huyo ambaye pia alikuwa Mwalimu wa Nidhamu alisimamishwa kazi Mei 28, mwaka huu, baada ya kikao cha uongozi wa shule kilichofanyika Mei 27 ambacho alimshirikisha Mkurugenzi wa shule.

Shani alisema uongozi wa shule ulipata malalamiko kutoka kwa mwanafunzi Mei 23, mwaka huu, kwa kuandika barua kuelezea usumbufu anaoupata kutoka kwa mwalimu huyo ambaye alimlazimisha awe na uhusiano naye na kufanya naye mapenzi mara kadhaa.

Alisema baada ya barua hiyo, uongozi wa shule ulimuita mwanafunzi na wenzake kuwahoji kuhusu suala la mwalimu huyo kuwa na mahusiano ya mapenzi na mwenzao ambao walithibitisha jambo hilo.

"Nilivyopata malalamiko kwa maandishi kutoka kwa mwanafunzi tulikaa kikao na Mkurugenzi wa Shule tukaamua kumsimamisha kazi Mei 28, mwaka huu," alisema.

Alisema suala hilo lilifikishwa hadi kwa Ofisa Elimu wa mkoa, Jeshi la Polisi na Dawati la Jinsia ambao wanaendelea kulifanyia kazi kwa taratibu nyingine za kisheria. Alisema uwezekano wa mwalimu huyo kurejea shule hapo kuendelea na kazi haupo kwa sababu tayari uongozi wa shule umeshachukua hatua za kuajiri walimu wengine ambao wameziba nafasi yake. Taarifa zaidi kutoka katika shule hiyo ambazo gazeti hili imezipata, awali mwanafunzi huyo baada ya kuwa amelalamikia kitendo anachofanyiwa na mwalimu huyo na uongozi wa shule kutochukua hatua, alilazimika kwenda ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida kupeleka malalamiko yake kwa Ofisa Elimu wa Mkoa.

Kabla ya taarifa kufikishwa mkoani, mwalimu anayetuhumiwa kufanya kitendo hicho alianza kumzushia makosa mwanafunzi huyo na kumpa adhabu kadhaa, ikiwa ni mbinu ya kumdhibiti asieleze suala la mahusiano yao kwa watu wengine.

"Mwalimu alianza kumwandama mwanafunzi (anatajwa jina) na kwa kumpa adhabu ya kulima majani, alimpiga hadi mkono ukavimba, visa vilikuwa haviishi," kilisema chanzo kimoja cha habari.

Taarifa zaidi zimedai kuwa mwanafunzi huyo aliitwa kwa mwalimu huyo usiku na kuamua kuwachukua wenzake ili washuhudie.

"Huyo mwanafunzi baada ya kuitwa kwa sababu aliona imekuwa kero alikwenda na wenzake wawili, mmoja alisimama dirishani na mwingine mlangoni, mwanafunzi alipoingia tu ofisini mwalimu alizima taa kwa hiyo mwanafunzi aliyekuwa mlangoni akagonga mlangoni na kujifanya ana shida ndipo mwalimu akaamua kuwasha taa na hakufanya lolote," kilieleza chanzo hicho.

Taarifa zaidi zimeeleza kuwa siku moja mwalimu huyo baada ya suala hilo kujulikana kwa kuwa alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nidhamu ya shule, aliamua kuitisha kikao cha kamati yeye mwenyewe mtuhumiwa, lakini baada ya kugundua suala hilo halijakaa vizuri kwa upande wake aliamua kukiahirisha ghafla wakati kilikuwa kimeshaanza.


Bank of India (Tanzania) Ltd.

Relationships beyond banking

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019

MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|---|
| | | USD | TSHS |
| 1.0 | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | **Up to** Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | **Over** Tshs 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | **Up to 5000 USD a day** | free | - |
| | **Over 5000 USD withdrawal** | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | - Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | - Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | - Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | **Deposit fee** | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |

OTHER DISCLOSURES
(VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 14.00% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 5.75% |
| | Over 6 months | 2.50% | 6.75% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.00% | 7.25% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 04.07. 2022 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 04.07. 2022 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 04.07. 2022 |

| No | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|---|
| | | USD | TSHS |
| 2.0 | **Savings Accounts** | | |
| a) | Saving bank customer ID Card-one time | 7 | 10,000 |
| b) | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 2,000 | 25,000,000 |
| c) | Cash withdrawal charges over USD 2,000 to 5,000 per day | 0.25% of withdrawal amount | |
| d) | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.60% of withdrawal amount | |
| e) | Cash withdrawal charges over TZS 25,000,000 per day | | 0.10% of withdrawal amount |
| f) | Required minimum opening balance | | |
| | Without Cheque book | 50 | 50,000 |
| | With Cheque book | 200 | 200,000 |
| g) | Monthly service fee | - | - |
| h) | Interim statement | 1.5 per page | 1500per page |
| i) | Cheque book charges 25 leaves | 15 | 20,000 |
| j) | Account closure | 25 | 35,000 |
| k) | **Maintenance of minimum account balance** | | |
| | Without cheque book | 50 | 50,000 |
| | With cheque book | 200 | 200,000 |
| l) | **Minimum balance charges (in case of non maintenance of minimum balance )** | | |
| | Without cheque book | 4 p.m | 900 p.m |
| | With cheque book | 15 p.m | 3,600 p.m |
| 3.0 | **Current Accounts** | | |
| | Ledger folio charges per folio (40lines per folio) | 4 per folio | 6,000 per folio |
| | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 5,000 | 25,000,000 |
| | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.6% of withdrawal amount | - |
| | Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| 4.0 | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |

| No | ITEM/TRANSACTION | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | | | |
| | - **Individual** | free | free | Free |
| | - **Corporate** | free | free | Free |

| No | ITEM/TRANSACTION | USD | | TSHS |
|---|---|---|---|---|
| e) | Others | - | | - |
| 5.0 | **Foreign Exchange Transaction.** | - | | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | | |
| | | A/C holder | Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 | 40 | – |
| | USD 6001-10,000 | 30 | | -- |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | | -- |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | | |

| No | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 6.0 | **Other Charges** | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | |
| | - **Individuals** | 3 | 5,000 |
| | - **Corporate** | 6 | 12,000 |
| 7.0 | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| 8.0 | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| 9.0 | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| 10.0 | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 04.07. 2022 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 04.07. 2022 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 04.07. 2022 |

216932901

# CRDB yatua DRC na dola milioni 30 sokoni

**Na Mwandishi Wetu,**
LUBUMBASHI

BENKI ya CRDB imekamilisha mipango ya kuzindua shughuli zake katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ikiwa na uwekezaji mahususi wa zaidi wa dola za Marekani milioni 30.

Taarifa iliyotolewa jana na benki hiyo, imetaja hatua hiyo ya kuwekeza katika nchi hiyo yenye wastani wa wakazi Sh. milioni 90, ni sehemu ya mkakati wake kujitanua kikanda unaolenga soko kubwa la Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uwekezaji huo wa CRDB huko DRC utakuwa na kitovu chake katika eneo la kibiashara la Lubumbashi na inatarajiwa kuanza kazi ndani ya nusu ya pili ya mwaka huu, baada ya kupewa baraka na mlezi wake, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mei 2021.

"Tunaiona DRC kama soko la kusisimua kwetu, kwani inatoa fursa ya kipekee kwa kundi letu kubadilisha maisha nje ya mipaka yetu," alisema Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mkuu wa CRDB.

Kimuundo, CRDB ndani ya DRC itakuwa na wanahisa wawili ambao ni Mfuko wa Uwekezaji wa Norway kwa Nchi Zinazoendelea (Norfund) na Mfuko wa Uwekezaji wa Denmark kwa Nchi Zinazoendelea (IFU).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, CRDB ndani ya DRC, itamiliki hisa kuu asilimia 55 wakati wanahisa waliotajwa kwa jumla watamiliki asilimia 22.5 kila mmoja.

Nsekela katika taarifa yake aliwataja wadau hao wa CRDB katika hisa, kuwa wako mahiri kibiashara na wana mtazamo endelevu katika maendeleo ya jamii.

Wawekezaji IFU wanatajwa kwamba wanawekeza katika kampuni yenye uwezo wa kifedha na kuchangia katika mabadiliko ya kijani na pia kujenga jamii yenye haki jumuishi.

Kwa upande mwingine, Norfund inatoa kipaumbele kwa uwekezaji katika maeneo manne ya uwekezaji yanayowiana na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Maeneo hayo ni pamoja na nishati, taasisi za kifedha, miundombinu ya kijani na biashara endelevu na zinazokua.

Ikiwa na eneo la ukubwa wa Ulaya ya Magharibi, DRC ndiyo nchi kubwa zaidi katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara (SSA). Ina maliasili nyingi, ikijumuisha madini kama vile kobalti na shaba, uwezo wa kufua umeme kwa maji, ardhi kubwa ya kilimo, bioanuwai nzuri na msitu wa pili kwa ukubwa duniani na wenye mvua.

"Tumefurahishwa na jinsi CRDB inavyojitolea kudumisha uendelevu na tunaona fursa kushirikiana na benki hiyo kuingia DRC kwani ni njia nzuri ya kukuza ushirikishwaji wa kifedha na kuchangia uzalishaji wa ajira katika nchi ambayo watu wengi hawana benki," alitamka Espen Froyn, Makamu wa Rais wa Norfund.

Vilevile, Makamu wa Rais wa IFU, Morten Elkjær, aliisifu CRDB kwa mvuto wake kibiashara, akipa wasifu wa kiongozi wa fikra na mshirika wa kimkakati hasa katika programu zake endelevu, ikiwamo kilimo kinachoendana na uhalisia wa hali ya hewa, nishati safi.

"Tunazingatia hasa uwekezaji ambao unasaidia mabadiliko ya kijani na kuchangia katika kupunguza umaskini na kuongeza usawa," Elkjær alisema.

CRDB inakuwa benki ya kwanza nchini kujitosa DRC, ikiwa na sura ya mshirika mkubwa wa kibiashara nchini humo katika sekta mbalimbali, kilimo hadi viwanda.

DRC kiuchumi inategemea Bandari ya Dar es Salaam, na mwaka wa 2019, ilitia saini na Tanzania katika makubaliano ya ujenzi wa reli ya kisasa 'Standard Gauge' inayounganisha pia Burundi.

Juzi, Rais Samia Suluhu Hassan alishuhudia utiaji saini wa ujenzi wa reli hiyo kipande cha Tabora-Isaka, ambao ni sehemu ya matarajio hayo ya kufika DRC.

Uwekezaji huo mpya DRC ni hatua nyingine, baada ya CRDB kufungua mradi kama huo katika nchi jirani ya Afrika Mashariki, Burundi mwaka 2012.




Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Ruvuma, Bakari Ally Mketo (kushoto), akikabidhi trekta kwa mkulima Chacha Marwa Mwikwabe, baada ya kufanikiwa kuwa mteja wa kwanza kupata mkopo kutoka Benki ya Biashara ya Taifa (NBC), kupitia huduma ya NBC Shambani, mjini Songea, mkoani Ruvuma jana. Wanne kulia ni Meneja wa Tawi la benki hiyo Songea, Frank Kiranga. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Bilioni 50/- kujenga mradi wa maji Ruangwa, Nachingwea

**Na Mwandishi Wetu,**
RUANGWA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imetoa Sh. bilioni 54 kwa ajili ya kugharamia mradi wa maji wa Chiuwe utakaohudumia wilaya za Ruangwa na Nachingwea.

Alibainisha hayo juzi jioni alipozungumza kwa nyakati tofauti na wananchi katika vijiji vya Mchenganyumba, Mbecha na Chimbila 'B' akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika Wilaya ya Ruangwa.

Majaliwa alisema maeneo mengi ya wilaya hiyo maji yake ni ya chumvi, hivyo serikali ilifanya utafiti na kubaini kuwa chanzo cha maji cha Chiuwe maji yake hayana chumvi na ni ya kutosha kuhudumia vijiji vya wilaya hiyo na wilaya jirani ya Nachingwea.

Alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais Samia kwa serikali kutoa kiasi hicho cha fedha kitakachowezesha kutekelezwa kwa mradi huo ambao kukamilika kwake, kutamaliza kero katika upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika wilaya hiyo.

Waziri Mkuu pia alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa Watanzania wote kujiandaa kuhesabiwa ikiwa ni pamoja na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa makarani wa sensa na viongozi wenye maeneo wanayoishi. Sensa ya Watu na Makazi imepangwa kufanyika nchini kote Agosti 23, 2022.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) wa Wilaya ya Ruangwa, Lawrence Mapunda, alisema mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ikihusisha vijiji 34 vya Wilaya ya Ruangwa na vijiji 21 vya Wilaya ya Nachingwea.

Mapunda alisema ujenzi wa mradi huo ambao unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2022/23, utakamilika mwaka 2025/26.

"Kwa sasa utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua ya ununuzi na unatarajiwa kukamilika baada ya miaka mitatu kwa awamu zote," alifafanua.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutamaliza tatizo la upatikanaji maji wilayani Ruangwa kwa zaidi ya asilimia 80. Chanzo cha maji cha Chiuwe kilichoko Nyangao kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 15 kwa siku huku mahitaji ya wilaya ya Ruangwa kwa siku ni lita milioni tisa.

# FEPT yaunga mkono utunzaji wa Loliondo

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Foundation for Environmental Protection in Tanzania (FEPT) imesema inaunga mkono jitihada za serikali kulinda ikolojia ya Loliondo, Ngorongoro na Serengeti isiharibiwe na shughuli za binadamu kama ufugaji na kilimo.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkurugenzi wa FEPT, Peter Mhagama, ilibainisha kuwa jitihada hizo zinalenga kuweka uwiano na matumizi sahihi ya ardhi katika maeneo hayo lazima yazingatiwe kwa maslahi mapana ya taifa.

"FEPT tunathamini maisha ya Watanzania wenzetu wanaoishi katika maeneo haya ya kwamba yanategemea matumizi ya rasilimali ardhi hiyo iliyowekwa kwa ajili yao kwa shughuli za kimaendeleo na tupo pamoja nao katika matumizi sahihi ya rasilimali hizo," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania na taasisi za kimataifa za uhifadhi kuungana na serikali ya kulinda mazingira kwa kuwa maliasili za taifa ni urithi wa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mhagama alisema umuhimu wa Pori Tengefu la Loliondo kwa Hifadhi ya Taifa Serengeti ni mojawapo ya maeneo ya urithi wa dunia na kwamba uhifadhi wa maeneo hayo ni muhimu ili kuinusuru ikolojia ya Serengeti.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kati ya eneo zima la Loliondo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 4,000, serikali imetenga eneo la kilomita 2,500 kwa ajili ya shughuli za wananchi, ikiwa ni sawa na asilimia 62.5 ya eneo zima.

Alisema eneo la kilomita za mraba 1,500 limetengwa na serikali kwa ajili ya uhifadhi kutokana na muhimu wake mkubwa kwa ikolojia ya Hifadhi ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

"Eneo hilo la kilomita za mraba 1,500 ni mazalia ya wanyamapori, vyanzo vya maji kwa ajili ya ikolojia ya Serengeti, mapitio ya wanyamapori wahamao kutoka Serengeti na Ngorongoro kwenda na kutoka Masai Mara, Kenya, ambayo ni ushoroba muhimu uliobaki katika ikolojia ya Serengeti – Ngorongoro – Masai Mara.

"Kwa pamoja tunaweza kulinda mazingira ya Loliondo na Ngorongoro na tunazitaka jamii zote kwenye maeneo hayo kukabiliana na tishio kubwa kwa uhifadhi wa wanyamapori Loliondo na Hifadhi ya Taifa Serengeti linalotokana na ongezeko kubwa la mifugo," alisema.

# Mabula azuia mkataba wa mashamba matatu

**Na Munir Shemweta,** MONDULI

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezuia mkataba wa upangishaji ardhi wa mashamba matatu, maarufu mashamba ya Steyn, yaliyoko wilayani Monduli mkoani Arusha ulioingiwa kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Monduli na Kampuni ya EBN Hunting Safaris.

Uamuzi huo umetokana na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli kuingia mkataba wa kufanya uwekezaji kwenye mashamba hayo ulioibua mkanganyiko baina ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli kutokana na Ofisi ya Msajili kutokamilisha wala kutoa shamba hilo kwa mtu ama mamlaka yoyote.

Hatua ya halmashauri kutafuta mwekezaji kwenye mashamba hayo ilitokana na ufutwaji mashamba uliofanywa na Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, kupitia tangazo la serikali la mwaka 2005 kwa lengo la upanuzi wa Mji wa Makuyuni. Mashamba ya Steyn ni muunganiko wa mashamba matatu ya Lente Estate, Amani na Loldebes yenye ukubwa wa ekari 15,163 yaliyoko wilayani Monduli ambapo katika kipindi cha miaka ya 70, raia waliomiliki mashamba hayo waliondoka nchini na kuyaacha kumilikiwa na Hermanus Steyn kupitia Rift Valley Seed Company Ltd.

Akitoa uamuzi huo baada ya kukagua mashamba hayo akiwa katika ziara yake ya siku mbili mkoani Arusha, Dk. Mabula alisema mashamba hayo kwa mujibu wa sheria ya masuala ya utwaaji yako chini ya umiliki wa Msajili wa Hazina, hivyo uongozi wa Wilaya ya Monduli ulitakiwa kuomba kibali cha matumizi ya eneo baada ya kutwaliwa.

"Kuanzia sasa halmashauri itambue eneo hili litakuwa chini ya usimamizi wa Maliasili na Utalii na wamewapa TAWA kwa ajili ya kuona namna ya kuliendesha," alisema Dk. Mabula. Alisema Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli alipaswa kujiridhisha kuhusu umiliki wa mashamba hayo kabla ya kuanza mchakato wa upangishaji uliohitimishwa na yeye pamoja na mwenyekiti wa halmashauri kutia saini mkataba huo.

Awali, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Isack Joseph, katika kikao cha ndani alimweleza Waziri wa Ardhi, Dk. Mabula, kuwa uamuzi wa halmashauri yake kuingia mkataba wa kukodisha mashamba hayo kwa mwekezaji ulitokana na halmashauri kutokuwa na chanzo chochote cha mapato cha uhakika. "Ukiangalia wilaya hii hakuna sehemu yoyote tunategemea kama wilaya. Kwa hiyo, tulipokaa na kutafakari kama baraza, tukaona kuna eneo ambalo serikali kimsingi liko chini yetu, kwanini tusiweke mikakati ya kutafuta mwekezaji ili tutengeneze fedha kwa ajili ya makusanyo," alisema.

Akielezea zaidi kuhusu utata wa uingiaji mkataba huo, Dk. Mabula alisema maombi ya awali ya kampuni ya EBN Hunting Safaris Ltd yalikuwa kupangishwa kwa kipindi cha miaka 30 lakini pamoja na muda kupunguzwa hadi miaka 18, bado hali hiyo haitoi uhalali wa mkurugenzi na mwenyekiti kutia saini mkataba ulioashiria shaka juu ya usalama wa rasilimali za taifa.

Mkataba kati ya halmashauri na kampuni ya EBN Hunting Safaris Ltd ulitiwa saini mwezi Mei 2022 na ulikuwa wa miaka 18 ambapo malipo yalikuwa kwa mwaka Sh. milioni 250 na iliamuliwa katika malipo hayo asilimia 60 ilipwe halmashauri na asilimia 40 ilipwe Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mashamba ya Steyn hajaendelezwa na ni mapori yenye wanyama mbalimbali kutoka ikolojia ya eneo husika kuzungukwa na maeneo ya Hifadhi za Taifa za Manyara, Tarangire na pori tengefu la Mto wa Mbu ambapo wanyama hutumia eneo hilo kama ushoroba.



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mang'onyi, wakati wa mkutano wa hadhara ambapo wananchi hao walimkataa mwenyekiti wao. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Wananchi wamkataa mwenyekiti kwa DC

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WAKAZI wa Kijiji cha Mang'onyi, Kata ya Mang'onyi wilayani Ikungi mkoani Singida wamemkataa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Issa Almas, mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Jerry Muro, kutokana na tuhuma mbalimbali ikiwamo ufujaji wa fedha.

Walichukua uamuzi huo jana wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini huko baada ya mkuu wa wilaya kuwasili na kuzungumza na wananchi ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kutembelea kata kwa kata na kijiji kwa kijiji kusikiliza kero za wananchi.

Wananchi hao walimweleza mkuu wa wilaya kwamba hawamtaki mwenyekiti huyo na ikiwezekana aondoke naye kwa madai ameshindwa kutatua kero za kijiji na pia amejihusisha na ufujaji wa fedha za kijiji.

Walisema kama hataachia nafasi yake hiyo, itakuwa ngumu kwao kushirikiana naye katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuwa hana ushirikiano na uhusiano mzuri na wanakijiji.

Kufuatia msimamo huo wa wananchi, Muro alilazimika kusimamia mchakato wa kiutaratibu wa kisheria na kikanuni wa kumwondoa mwenyekiti huyo madarakani.

Mkutano wa kijiji uliketi papo hapo na kupiga kura 12 zilizomkataa mwenyekiti huyo ambapo baada ya zoezi hilo kukamilika, wananchi walipendekeza majina ya wananchi wawili ambao walipigiwa kura ya kukaimu uenyekiti wa kijiji.

Katika mchakato huo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mang'onyi Stendi, Elineema Mtinangi, ndiye alifanikiwa kupata kura nyingi zilizomwezesha kuchaguliwa kukaimu nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Mang'onyi hadi hapo uchaguzi wa serikali za mitaa utakapofanyika.

Baada ya mabadiliko hayo, Mkuu wa Wilaya, Muro, alianza kutatua kero ya maji kwa kuagiza wataalamu wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) kufika kijijini na kurekebisha kisima cha Taru milimani ili wananchi wapate maji.

Muro pia aligiza wataalamu kufanyika tathmini ya hali ya athari za kilimo katika msimu huu kuanzia ngazi ya kijiji na kubaini kaya ambazo zitakuwa na upungufu wa chakula ili serikali zianze kutafutiwa msaada wa chakula haraka.

## Waziri ashtukia jambo fursa za masoko ya nje

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amesema imefika wakati wa mamlaka za biashara nchini, ikiwamo sekta binafsi na wafanyabiashara wengine, kuanza kuona umuhimu wa kuyafikia masoko ya nje wenyewe moja kwa moja badala ya kuwatumia majirani wanaowadidimiza kibiashara.

Aliyasema hayo usiku wa kuamkia jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa mapokezi ya Baraza la Biashara la Tanzania na Pakistan, akibainisha kuwa kuna baadhi ya majirani wanachukua bidhaa nchini, ikiwamo vyakula, na kwenda kuandika kwamba zimezalishwa kwao, jambo ambalo si sahihi.

Naibu waziri huyo alisema kuna baadhi ya bidhaa ambazo huuzwa nchi jirani ambazo huchukuliwa na kwenda kuuzwa katika mataifa mengine na kutengeneza faida mara 100 ya ile thamani waliyoipata wafanyabiashara wa Tanzania.

"Tunaweza kushirikiana kwa faida ya pande zote mbili kati ya Tanzania na Pakistan, kumekuwa na maneno ya kuambiwa na matokeo yake wale wenzetu madalali wamekuwa ndiyo wanaofaidika na bidhaa ambazo wanatoa kwetu na kuuza Pakistan, tuone umuhimu sasa wa kuyafikia masoko hayo sisi wenyewe. "Mimi ninaamini wafanyabiashara wa Tanzania tunaweza kuingia kwenye masoko haya ikiwamo hili la Pakistan ambao wako tayari kushirikiana na sisi, na ni muda mwafaka sasa kama tumeamua kushirikiana na wenzetu tuhakikishe tunaanza kuingia kwenye masoko hayo," alisema Kigahe.

Aliongeza kuwa wafanyabiashara waone pia ni namna gani ya kupata bidhaa kutoka Pakistan ikiwamo vifaa vinavyotumika katika hospitali na kwenye kilimo ambavyo vinachukuliwa kwa bei rahisi na mataifa mengine na kuiuzia Tanzania kwa gharama kubwa, huku akisisitiza Watanzania kuitumia fursa hiyo vizuri.

Alibainisha kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ametaka kuiwezesha sekta binafsi iwe ndiyo sekta kiongozi katika kujenga uchumi wa Tanzania, na kwamba katika mpango wa miaka mitano wa maendeleo, wanataka kuwe na ushindani wa viwanda kwa maendeleo ya Watanzania.

Pia alisema wanataka kuwa na uchumi jumuishi na mwenye kutimiza malengo hayo siyo serikali, bali sekta binafsi, huku akisisitiza kuwa kwa kushirikiana na mabaraza ya biashara na nchi mbalimbali, ikiwamo Pakistan, wanaweza kufikia uchumi wa ushindani kwa kushirikishana fursa zilizoko na kupata vifaa na mitambo itakayosaidia kuzalisha bidhaa zenye ubora.

"Ili tupate ushindani ni lazima tuhakikishe tunashirikiana na watu ambao wana upendo wa dhati kuhakikisha tunapeana au tunapata zile fursa ambazo ni sahihi na za moja kwa moja, niahidi kwamba serikali itaendelea kushirikiana na Serikali ya Pakistan katika kufanya maendeleo na baraza la biashara kati ya Tanzania na Pakistan limezinduliwa rasmi," alisema Kigahe.

Balozi wa Pakistan nchini, Muhammad Saleem, aliahidi kuwa serikali ya nchi hiyo itaendelea kushirikiana na Tanzania katika nyanja mbalimbali ikiwamo elimu, uchumi na biashara na kuleta maendele endelevu kwa manufaa ya pande zote mbili.

# Chuo Kumbukumbu Mwalimu Nyerere kufundisha uongozi

**Habari zote na Elizabeth Zaya**

CHUO cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kimesema kinatarajia kuanza rasmi ufundishaji wa programu mpya ya masomo ya uongozi, maadili na utawala bora kuanzia ngazi ya cheti hadi shahada katika mwaka mpya wa masomo.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Prof. Richard Kangarawe, katika banda la chuo hicho kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), yanayoendelea kwenye viwanja vya Sabasaba.

Prof. Kangarawe alisema lengo la kuanzisha programu hiyo ni kuhakikisha kuwa kinatoa na kuandaa viongozi wazuri na bora wa baadaye.

Alisena dira ya chuo hicho ni kuwa kitovu cha utoaji wa maarifa bora kwa kutoa elimu na mafunzo ya kibunifu na uvumbuzi pamoja na kuendeleza amani na umoja wa kitaifa.

"Chimbuko la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni Chuo cha Kivukoni ambacho kilianzishwa rasmi Julai 29, 1961, uamuzi wa kuanzishwa kwake ulikuwa ni Mkutano Mkuu wa Chama cha TANU uliofanyika Tabora mwaka 1958, na miongoni mwa malengo yake ni kuhakikisha kinatoa viongozi waliopikwa vizuri," alisema Prof. Kangarawe.

"Kwa hiyo tutahakikisha kwamba chuo hiki kinaendelea kuwa kitovu cha kuzalisha viongozi wetu wazuri katika nchi hii, ambao watalitumikia taifa kwa weledi na uzalendo."

Aliwataka Watanzania kutembelea banda lao kwenye viwanja vya maonesho hayo ili wajifunze mambo mbalimbali.

"Wapo ambao hawafahamu kwamba katika kipindi cha mwaka 1972 hadi 1992 chuo hiki kilikuwa chini ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na kilikuwa na vyuo vya kanda nane katila Jamhuri ya Muungano na nchi yetu ilipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992 chuo kilianza kumilikiwa rasmi na serikali kupitia Wizara ya Elimu, yote hayo watayafahamu wakija," alisema Prof. Kangarawe.

"Chuo kilipewa jina la Mwalimu Nyerere kwa lengo la kuendelea kumuenzi Baba wa Taifa ambaye alifanya kazi kubwa ya ukombozi wa taifa letu, ukombozi wa Afrika na kuwatetea wanyonge popote duniani, kwa hiyo hivi vyote Watanzania wanapaswa kuvifahamu."




Ofisa wa Barrick Tanzania, Amedeus Swai (kulia), akitoa maelezo ya shughuli za kampuni hiyo kwa wananchi waliotembelea banda la kampuni kwenye maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TPDC kuongeza upatikanaji wa gesi asilia majumbani

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), limesema linaendelea kufanya utafiti wa kuongeza upatikanaji wa gesi asilia majumbani.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa Uhusiano wa Shirika hilo, Francis Lupokelo, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho hayo.

Alisema tayari serikali imeruhusu Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) na Shirika hilo kushirikiana kwenye kutoa pesa ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya kusambaza gesi hiyo.

"Kwa bahati nzuri sana ni kwamba serikali imeruhusu Wakala wa Umeme (REA) kushirikiana na TPDC kwenye kutoa pesa, ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia na tayari timu hizi zimeshafanya kazi ya awali katika maeneo ya Pwani pamoja na Lindi," alisema Lupokelo.

Alisema mpaka sasa viwanda vinavyotumia gesi asilia ni 45, nyumba 1,500, taasisi mbili, shule nne na magari 1,400.

"Hayo ndiyo maendeleo ambayo tumeyafikia mpaka sasa kuhusiana na suala la wananchi kutumia gesi asilia japokuwa bado tunaendelea kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali," alisema Lupokelo.

"Na haya ndiyo mambo tunayowaeleza wananchi wanapofika kutembelea uhakika wa upatikanaji wa gesi hiyo asilia, tunaonyesha kuhusu ni namna gani watanufaika."

Pia, alisema wataendelea kuunganisha gesi asilia kuhakikisha kwamba inafika katika maeneo ya mikoani pamoja na kutengeneza mazingira ya kuisindika.

"Kwa sababu tunajua ujenzi wa miundombinu ulivyo mgumu, kwa hiyo njia za harakaharaka ambazo zinaweza kufanyika ni kusindika gesi ili matumizi yaendelee," alisema Lupokelo.

"Kama tunakumbuka juzi tuliingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ili kukodishwa eneo ambalo litakuwa linatumika kujenga kituo kikubwa cha kusindika gesi. Hii maana yake ukiwa na kituo kikubwa unaweza kuhudumia vituo vidogo vidogo vingi. Na hii pia itasaidia matumizi ya gesi kwa kiwango kikubwa katika viwanda.

## Wazawa wachangamkia fursa sekta nishati gesi

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mkondo wa juu wa Petroli (PURA), imesema ushiriki wa wazawa katika kuchangamkia fursa zinazopatikana kwenye sekta hiyo umeongezeka zaidi huku idadi ya wanaoajiriwa na kampuni za gesi asilia ikiongezeka hadi kufikia asilimia 90.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Kitengo cha PURA, Charles Nyangi, kwenye maonyesho ya DITF yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba.

Alisema asilimia 60 ya watoa huduma wakiwamo wasambazaji wa bidhaa hizo za gesi asili pamoja na malighafi kwa sasa zinafanywa na Watanzania na asilimia 40 pekee ya fursa zinazopatikana katika sekta hiyo ndiyo zinafanywa na kampuni kutoka nje.

Nyangi alisema kutokana na mwitikio huo, PURA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeamua kuandaa kazindata ya kusaidia wataalam mbalimbali wa masuala ya mafuta na gesi kupata ajira kwa urahisi zaidi.

"Kupitia fursa mbalimbali zinazopatikana, tumeanzisha kanzidata kwa kushirikiana na EWURA ambayo itatusaidia kuandaa wataalamu na kuwatambua kwa njia rahisi zaidi pale kunapopatikana ajira," alisema Nyangi.

"Kanzidata hii imeanza kutumika tangu mwezi Mei, mwaka huu na tumeanza kuandikisha kupitia website (tovuti) yetu na fomu maalum, lengo ni kuhakikisha kwamba hawakosi fursa pale zinapopaikana."

Alisema katika maonyesho hayo wanatoa elimu kuhusu mambo mbalimbali ikiwamo elimu ya kazi wanazofanya ili wananchi waweze kuzitambua na kuzijua katika utafutaji, uchimbaji na usambazaji wa gesi na petroli.

## Maonyesho dhahabu yapandishwa hadhi

SERIKALI imeyapandisha hadhi maonyesho ya dhahabu yanayofanyika Septemba ya kila mwaka mkoani Geita na kuwa ya kitaifa.

Kutokana na kupanda hadhi Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade) imeingia makubaliano na mkoa wa Geita wa kuyaendesha kwa hadhi hiyo ya kitaifa.

Akizungumza wakati wa utiaji saini wa makubaliano hayo uliyofanyika katika Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, alisema makubaliano hayo ni kwa ajili ya kuweka nguvu kubwa ya kuyaboresha.

Alisema yatasaidia kukua na kuwavutia wawekezaji wengi ndani na nje ya nchi kushiriki kuonyesha bidhaa zao.

"Tunafahamu kuwa muda uliobakia ni mchache kwani Septemba ndiyo yatafanyika maonyesho ya dhahabu mkoani Geita, tumeshawaambia wadau kuwa hatutayapeleka mbele hivyo kwa kushirikiana na Tantrade tutakaa pamoja na kukubaliana namna bora ya kuyaboresha ili yaonekane ya hadhi na kisasa," alisema Senyamule.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Geita, Zahra Michuzi, alisema makubaliano hayo yatasaidia kuleta mapinduzi na kufanya mabadiliko kwenye teknolojia ya dhahabu ndani na nje ya mkoa huo.

"Tunataka kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya madini ya dhahabu, kwahiyo kupanda hadhi kwa maonyesho hayo kutachagiza mabadiliko kwenye sekta hiyo," alisema Zahra.

Mkurugenzi Mtendaji wa TanTrade, Latifa Khamis, alisema kutiwa saini kwa makubaliano hayo kutaimarisha na kusaidia uwanja wa maonyesho wa Geita kuwa wa kisasa kwa ajili ya maonyesho hayo ya dhahabu.



Ukurasa 12

**Kuelekea katiba mpya, BAWACHA iko na Rais**



Ukurasa 13


Tofauti za kisiasa Ruto na bosi wake Uhuru, isiwe kigezo nani atashinda


siasa

JUMATANO JULAI 6, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 14

**Patrice Lumumba azikwa rasmi DRC**

KATIBA MPYA

# Ianze na enzi za kuitii, kuiheshimu

**Na Mwandishi Wetu**

KUANDIKWA katiba mpya kwa Tanzania ni jambo linaloelezwa kuwa ni hitaji la taifa ili kutekeleza mageuzi ya kidemokrasia na ya uchumi wa 'kiliberali' kwa sababu katiba ya sasa kwa miongo mingi haikidhi mahitaji hayo.

Tena inaeleza kuwa itikadi ya Tanzania inayotajwa na katiba ni ya 'ujamaa na kujitegemea' japo taifa linafuata uchumi na siasa za kiliberali.

Ujio wa katiba mpya unaelezwa kuwa utaleta mabadiliko ya kuiongoza serikali, utamaliza miongo kadhaa ya utawala unaompa rais madaraka makubwa ya kuteua viongozi na watendaji wakuu karibu wote na kufanya majukumu mengi makubwa ya kitaifa bila kuhojiwa, lakini hata anapoondoka madarakani hashitakiwi.

Dhana ya katiba mpya inatarajiwa kuwa ni kuwapo kwa uhuru wa vyama vingi vya siasa, uchaguzi huru, mahakama huru, taasisi huru kama tume ya uchaguzi, ofisi ya vyama vya siasa yote hayo ni miongoni mwa mabadiliko muhimu yanayotarajiwa kuletwa na katiba hiyo kidhahania.

Tatizo linaloonekana kwenye katiba mpya za Afrika ikiwamo ya Tanzania ni kuwapo kwa 'katiba' zisizo na utii wa katiba," yaani inatokea maamuzi mengine yakafanyika na serikali bila kujali kuwa yanakwenda kinyume na katiba.

Hilo ndilo ambalo linalalamikiwa,katiba inaruhusu vyama vingi lakini mikutano ya vyama vya siasa hairuhusiwi .

Hiyo inabainisha kuwa kuna haja ya kutaka mapambazuko mapya kisiasa na kuwa na enzi mpya zinazoondoa walakini kama wa kuwa na katiba lakini zikawapo mamlaka zisizoifuata.

Katiba mpya ni muhimu ili kuachana na uendelezaji wa baadhi ya mambo kama hayo ambayo yanakuwa kama uundaji na urejeshaji wa utawala wa kale unaoendelea kuleta ukinzani wa siasa za vyama vingi na uhuru wa kidemokrasia.



Waziri wa Sheria na Katiba, Dk. Damas Ndumbaro. **PICHA: MAKTABA**

Aidha, katiba hiyo mpya ni hitaji la msingi ili kuondoa utaratibu wa uongozi wa serikali za mitaa na wa bunge la chama kimoja. Vyombo hivyo vinaingia madarakani bila kuwapo na diwani, kiongozi wa serikali mtaa au mbunge wa kutoka upinzani.

Sababu zinaweza kuwa kuenguliwa kwa madai ya kushindwa kuandika majina yao au kukosea baadhi ya vipengele kwenye fomu walizojaza kushiriki uchaguzi.

Licha ya kwamba ilipofika miaka ya mwanzo ya 1999, Tanzania kama mataifa mengi ya Afrika iliruhusu ushindani wa vyama vingi kuanzia wabunge, urais na serikali za mitaa , malalamiko kwenye usimamizi wa uchaguzi hayajawahi kuacha kusikika, kilio kikielekezwa kwenye tume ya uchaguzi, ambayo mzizi wake ni katiba iliyopo.

Uchaguzi wa vyama vingi vya siasa uliofanyika nchini umekuwa mara kadhaa chanzo cha malalamiko figusu wakati wa kutangaza matokeo na wakati mwingine kuwepo na kesi nyingi.

Wengi wanaona kuwa ufumbuzi wa changamoto za kidemokrasia ni kuwa na katiba mpya lakini bado swali linabakia pale pale je katiba hiyo itatoa fursa sawa kwa upinzani na chama tawala? Vipi suala la kuwa na mahakama huru? Vipi uhuru wa asasi za kiraia, vyombo vya habari na kigugumizi cha maslahi ya taifa?.

Swali muhimu ambalo linahitaji kujibiwa, na ambalo ni muhimu ni kuwa na kuhakikisha kuwa kunakuwa na katiba ambayo kila raia ataitii na kudumisha demokrasia na ambayo inaweza kushughulikia changamoto mbalimbali za kitaifa na kijamii na kiuchumi ili kuleta maendeleo

Kwa Tanzania ikumbukwe kuwa majeruhi wa kwanza baada ya Uhuru mwaka 1961 ni demokrasia ya vyama vingi. Hivi vilifutwa na kama nchi nyingine za Afrika baada ya ukoloni wengi walipinga siasa za vyama vingi kwa maelezo mbalimbali.

Ilichukuliwa kama aina ya siasa, yenye asili ya Magharibi au ya kikoloni na ngeni kwa utamaduni wa kiasili za Afrika, ambazo zilisemekana kuwa na upendeleo wa kujenga maelewano yasiyo na upande wowote wala mgawanyiko wa kivyama.

Hivyo hata Watanzania walizidi kukataa vyama vingi na kutaka chama kimoja. Hata mwishoni mwa miaka ya 1980 waliendelea kusema kuwa hawataki vyama vingi , lakini serikali ikakubali maoni ya wachache na kurejesha rasmi mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Kwa hiyo licha ya kutaka katiba mpya ni lazima Watanzania na uongozi uzingatie katiba na kukubali kubadilika ili uhalali wa kila jambo usimamiwe na katiba kulinda masuala muhimu ya ustawi wa raia, uchumi, siasa, haki na kupata maendeleo.

Suala la kuwa na katiba mpya ni muhimu lakini ni lazima serikali iridhie kuwa sasa ni wakati wa mageuzi ya kikatiba, kisheria, kidemokrasia,uhuru wa kujumuika wa asasi za kiraia, uhuru wa vyombo vya habari , vyama vya upinzani na mahakama.

Ili katiba iwe na kile watu wanachokitamani ni lazima itokane na maoni ya raia lakini pia iondoe 'figisu' zinazolalamikiwa wakati wote hivyo ikidhi matakwa ya demokrasia ya siasa za vyama vingi.

# Kuelekea katiba mpya, BAWACHA iko na Rais

## • Yamtabiria kufanikisha mchakato kikamilifu

**Na Sabato Kasika**

NI majira ya mchana, alipowasili katika ofisi za gazeti hili, huku muonekano wake wa mwanzo si sehemu ya wageni wa kawaida ambao wamezoeleka ofisi hizi, anaonekana anayejiamini na mwenye kumfurahia kila mmoja.

Baada ya utambulisho na mawasiliano kidogo, wasifu na muonekano wa mgeni huyo, unahama katika sura ya kipekee, ambayo inapata uthibitisho kupitia namna anavyojieleza, kujiamini, na nafasi maalum anaonyesha kukifahamu ndani nje, chama chake cha CHADEMA.

Akibeba upekee mwingine, ndiye aliyebebeshwa jukumu la kukaimu uongozi wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA -BAWACHA.

Huyo ni Sharifa Suleiman, ambaye sasa anakuwa sehemu ya kinachosisitizwa na chama chake.

Kadhalika kwenye kudai nchi kupata katiba mpya, hasa baada ya chama tawala- CCM kuungana na hoja aliyosema ni ya 'kwao', mwelekeo wa kisiasa nchini, ili ubarikiwe na uwapo wa katiba mpya.

Ni jambo analosimama nalo,katika mazungumzo yake na gazeti hili wiki iliyopita, kiongozi huyu wa BAWACHA ambaye ni mwanahabari aliyefanya kazi za utangazaji wa redio mjini Zanzibar.

Akiwa msomi wa masuala ya utawala wa umma Sharrifa aliyejiunga na CHADEMA, akiwa Zanzibar anaeleza kuwa

CCM kuunga mkono kilio cha kuwa na katiba mpya, anasema anaamini Rais Samia Suluhu Hassan, atafanikisha mchakato.

"Binafsi sina shaka na Rais Samia kwenye suala la kupatikana kwa katiba mpya, hivyo ninaamini kuwa hatua ya CCM chini yake wa kuutangazia umma uamuzi mpya kuhusu suala la katiba, utazaa matunda," anasema Sharifa.

**IMANI KWA RAIS**

Sharifa anafafanua kuwa Rais mstaafu Abeid Aman Karume, alifanikisha Zanzibar kuwa na katiba mpya, na kwamba Rais Samia ni mwanafunzi wake wa siasa, hivyo anaamini ataiga kutoka kwa mwalimu wake.

"Siwezi kushangaa kuona akiiga nyayo za mwalimu wake, ili kuwapa Watanzania Katiba Mpya kama ambavyo Karume aliwapa Wazanzibari katiba mpya ambayo inaendelea kutumika hadi sasa," anasema.

Anafafanua kuwa pamoja na kwamba bado miaka michache kufikia uchaguzi wa mwaka 2024/2025, kupatikana katiba mpya ni suala la wadau kujipanga na kukubaliana na kuwapa Watanzania kile wanachokitaka.

Anasema, suala la kuwapo katiba mpya si hitaji la chama fulani bali ni takwa la nchi, na kwamba wadau wakiwamo wanasheria, wanasisa na wengine wakishirikiana mchakato unaweza kufanyika haraka ili uchaguzi ujao katiba hiyo itumike.

"Ninaamini kwamba, Rais Samia anaweza kuharakisha kuwapa Watanzania kile wanachohitaji, kwani ni mwanasiasa aliyeiva, lakini pamoja na hayo, nimuombe asirudi nyuma kusimamia mchakato huu," anasema.


Anasema, baadhi ya wanasiasa wanaweza kushangaa uamuzi mpya wa CCM kuhusu katiba mpya, na kwamba mazingira ya siasa yaliyokuwapo miaka sita iliyopita, hayakuruhusu kujadiliwa kwa suala hilo.

"Mimi ninaamini kuwa msimamo wa Rais Samia ni sawa na ule wa Karume kwenye suala la katiba, unafanana, ila wasitokee wanasiasa kwa maslahi yao, wakapenyeza mambo ya kukwamisha mchakato huo," anasema.



Sharifa Suleiman, Kaimu Mwenyekiti wa BAWACHA Taifa. **PICHA: SABATO KASIKA**

> Bahati nzuri CHADEMA ina hazina kubwa ya wanawake wenye uwezo wa kuongoza, ndiyo maana tunafanya ziara ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kuwania uongozi ili waonyeshe uwezo wao.




**BAWACHA IMARA**

Anasema, pamoja na kwamba baraza hilo limepitia changamoto kadhaa ikiwamo sakata la wanachama 19 kufutwa uanachama, bado liko imara zaidi ya ilivyokuwa miaka ya nyuma, na kwamba linachapa kazi kama kawaida.

"Siasa ni vita, watu unaowaamini wanaweza kukusaliti kama ilivyotokea kwetu, lakini sioni umuhimu wa kuwazungumzia wale waliotusaliti, itakuwa ni sawa na kuonyesha kuwa bado wanahitajika, bali tuzungumze kile tunachokifanya viongozi wa BAWACHA," anasema.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, alikuwa akitokea mikoa ya kanda ya ziwa na kanda ya Kigoma, kanda ya kati mkoani na kumalizia Dar es Salaam, anasema baraza hilo na chama kwa ujumla wako imara zaidi.

"Naomba nikuhakikishie kuwa BAWACHA iko imara zaidi ya jana, imekuwa ni tofauti na jinsi ambavyo wale wasioitakia mema wamekuwa wakikusudia, tunaendelea kuhamasisha na kuimarisha chama na jumuiya zake," anasema.

Anasema ziara zake mikoani zimekuwa zikiendelea kuzaa matunda kwa kusajili wanachama wapya wengi kupitia 'Tunasonga Kidigitali', na kwamba Watanzania wakiona chama hicho kama mkombozi wao kwa sera zake.

**UJUMBE KWA WANAWAKE**

Sharifa anawapa ujumbe wanawake kwamba, waendelee kujiandaa kuwania uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na mkuu unaofanyika 2025, akieleza kwamba huu ni wakati wao kwa kuwa hata Rais wa nchi ni mwanamke.

Anasema, wanawake ni jeshi kubwa, ambapo anawataka wasibaki kuendelee kuwa wapigakura tu, bali wawanie nafasi za uongozi, kwa kuwa wanaweza kuongoza kama ambavyo Samia ameonyesha mfano.

"Ni wakati wetu wanawake, 'tusilaze damu', badala yake tujipange kwa ajili uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na kisha uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani mwaka 2025," anasema.

Sharifa anasema, wanaweza kudhani kuwa mwaka 2024 na 2025 bado ni mbali, lakini anawakumbusha kuwa mwisho wa uchaguzi mmoja ni mwanzo wa uchaguzi mwingine, hivyo anawahimiza waendelee kujiandaa.

Kaimu mwenyekiti huyo anasema huu si wakati tena wa wanawake kubaguana kivyama, badala yake waangalie yule ambaye wanaona anafaa kuongoza, wamchagüe kwa kura za kishindo ili awaongeze.

"Bahati nzuri CHADEMA ina hazina kubwa ya wanawake wenye uwezo wa kuongoza, ndiyo maana tunafanya ziara ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kuwania uongozi ili waonyeshe uwezo wao," anasema Sharifa ambaye kitaaluma ni mwanahabari, mtaalamu wa masuala ya utawala wa umma na siasa.

KINYANG'ANYIRO CHA URAIS KENYA...

# Tofauti za kisiasa Ruto na bosi wake Uhuru, isiwe kigezo nani atashinda



Wanasiasa Jaramogi Oginga baba wa Raila Odinga (kushoto) na Mwasisi wa Kenya Jommo Kenyatta, baba wa Rais Uhuru Kenyatta, katika majukwaa ya uongozi miongo kadhaa iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

**Na Damian Mnyikwa, SJMC**

AGOSTI 9, mwaka huu Kenya itafanya uchaguzi mkuu kupata magavana, wabunge na rais watakaoongoza taifa hilo lenye uchumi mkubwa katika ukanda wa Afrika mashariki kwa miaka mitano ijayo.

Macho na masikio ya wana Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa wafuasi wa masuala ya siasa yapo nchini humo yakifuatilia kila hatua kuhusu uchaguzi wa taifa hilo ambalo linatajwa angalau kuwa limestawi kidemokrasia ikilinganishwa na mataifa mengine.

Uchaguzi huu ni mwendelezo wa uchaguzi katika mataifa ya Afrika mashariki katika miaka ya hivi karibuni ikikumbukwa Tanzania na Burundi zilifanya uchaguzi mwaka 2020, Uganda mwaka 2021 huku Congo ambaye ni mwanachama mpya wa jumuiya hiyo akitarajiwa kufanya mwaka ujao.

Aidha taifa jirani na Kenya la Somalia limefanya uchaguzi wake mwaka huu.

Uchaguzi mkuu nchini Kenya hutazamwa kwa jicho la tatu katika ukanda huu, ukitajwa na wengi kuwa mfano kutokana na kiwango cha demokrasia kinachoshuhudiwa. Lakini licha ya hilo uchaguzi wa mwaka huu umechukua sura na mvuto wa aina yake kutokana na mambo mengi.

Ni mara chache sana kwa mataifa ya Afrika, kiongozi

> Ikiwa Raila Odinga atafanikiwa kuwa rais wa Kenya katika uchaguzi huu, basi mtangulizi wake Uhuru Kenyatta atakuwa amelipa deni kubwa la kisiasa ambalo lilipaswa kulipwa na baba yake.



Raila Odinga



Uhuru Kenyatta

wa serikali kumuunga mkono mgombea wa upinzani. Bila kupepesa macho Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya ambaye ni mwenyekiti wa chama tawala Jubilee ameapa mbele ya umma kuwa atamnadi Raila Odinga hasimu wake wa zamani kisiasa kutoka chama cha upinzani ODM (sasa muungano wa umoja) katika kampeni za urais.

Sababu zinatajwa na wengi kuwa Makamu William Ruto alikaidi maagizo yake mengi hasa ya watumishi wa serikali kuachana na siasa tangu mwaka 2018 badala ya kuwatumikia wananchi.

Utofauti baina ya wawili hawa waliokuwa katika chama tawala cha Jubilee uliibuka mwaka 2018 baada ya makubaliano ya kuleta amani nchini Kenya maarufu kama "Handshake" kati ya Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa chama cha Upinzani ODM Raila Odinga.

Kwa mfano wakati ripoti ya makubaliano yao ya kuleta amani inazinduliwa Novemba mwaka 2019 katika ukumbi wa Bomas Makamu Rais William Ruto hakupewa nafasi ya kushiriki mkutano baina ya Uhuru Kenyatta na Raila Odinga jambo lilotafsiriwa na wafuasi wake kuwa alifedheheshwa.

Kumekuwa na mfululizo wa mambo mengi ya hapa na pale yenye tofauti baina ya viongozi hawa ambayo unaweza kusema kuwa hawapikiki chungu kimoja.

Ndiyo maana Uhuru Kenyata ameshindwa kumuunga mkono makamu wake na badala yake kumgeukia aliyekuwa hasimu wake kisiasa.

Hii ni moja ya sababu, nyingine kubwa inatajwa kuwa Uhuru Kenyatta anarudisha fadhila kwa niaba ya baba yake mzazi Jommo Kenyatta kwa hayati Mzee Jaramogi Ajuma Oginga Odinga baba mzazi wa Raila Odinga.

Inatajwa kuwa hayati Mzee Jaramogi Oginga na hayati mzee Jomo Kenyatta walikuwa marafiki wa karibu wakati wa harakati za kupigania uhuru ikielezwa kuwa wakati Kenya inapata uhuru wake mwaka 1963 hayati Mzee Odinga alikuwa na nafasi kubwa ya kuwa rais wa kwanza wa Kenya lakini kwa kutambua nafasi na umuhimu wa Jomo Kenyatta (akiwa ametoka gerezani), alikubali kumwachia kiti hicho na yeye akawa makamu wake wa kwanza.

Ingawa wengi wanadai hii ilikuwa sababu ya ukabila, kutokana na ushawishi wa kabila la Wakikuyu ambao walipigana vita vya Maumau ambapo ili kuweka mambo sawa basi walipaswa kuongoza nchi.

Kitendo cha Rais Uhuru Kenyata kumuunga mkono Raila Odinga kinadhihirisha hoja za wengi kuwa anajaribu kurudisha shukrani kwa kile kinachoweza kuelezwa kuwa isingelikuwa matakwa ya hayati mzee Odinga basi baba yake mzee Jomo Kenyata asingelikuwa Baba wa Taifa wa Kenya.

Ikiwa Raila Odinga atafanikiwa kuwa rais wa Kenya katika uchaguzi huu, basi mtangulizi wake Uhuru Kenyatta atakuwa amelipa deni kubwa la kisiasa ambalo lilipaswa kulipwa na baba yake.

Siasa za ukabila bado ni tishio kwa taifa hilo Kabila kubwa la Kikuyu bado linataka kuhodhi madaraka na wanaamini kuwa wao ndio wanapaswa kuwa katika mamlaka za juu za uongozi.

Haya ni madhara ya ukoloni ambao waliyaweka baadhi ya makabila katika ngazi ya utawala na mengine yakabaki katika ngazi ya utumishi na uzalishaji, changamoto hii imesalia kuwa mwiba kwa nchi nyingi za kiafrika.

Pengine, wana Afrika Mashariki wana imani wananchi wa Kenya hawatotumia mgogoro baina ya Rais Uhuru Kenyatta na naibu wake William Ruto kuwa kigezo cha kumpata rais wao. Chama kitakachonadi sera zake kikamilifu kinapaswa kupewa nafasi na kutwaa madaraka.


Haijalishi ni William Ruto, Raila Odinga ama mgombea yeyote yule sera zake ndizo zinapaswa kusikilizwa na kumpa nafasi ridhaa ya wananchi. Endapo hili litafanikiwa hapana shaka taifa la Kenya litakuwa limepiga hatua nyingine kubwa kidemokrasia na kuyaacha mataifa mengine katika ukanda wa Afrika mashariki yakijikongoja katika kuimarisha demokrasia zao hasa katika masuala ya uchaguzi.

*Maoni: 0754358915, mnyikwas@gmail.com*

JUKWAA LA VIONGOZI

# Lumumba azikwa rasmi DRC

## • Ni baada ya miaka 61, kilichozikwa jino



Askari watesi wa Patrice Lumumba wakimsulubu kabla ya kumuua miaka 61 iliyopita. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imeadhimisha shamrashamra za kuadhimisha miaka 61 ya uhuru wake.

Zilishuhudia mazishi ya shujaa wa uhuru wa Congo Patrice Lumumba, akizikwa lakini kilichozikwa ni jino lake la dhahabu, mazishi yakifanyika jijini Kinshasha miaka 61 baada ya kifo chake, akidaiwa kuuawa na waasi waliotaka kujitenga wakiungwa mkono na Ubelgiji na mataifa ya Magharibi.

Kuna maelezo kwamba, kampuni ya madini ya shaba Zaire au DRC ya Union Miniere du Haut Katanga, ilihusika kwa karibu na kuuawa Lumumba kwa mkono wa Kanali Joseph Mobutu, akiwa na askari wa kukodiwa.

Ndivyo uhuru wa DRC unavyoazimishwa kwa kurejea mauaji ya kikatili ya Lumumba.

Mamia ya Wakongo walikusanyika katika uwanja mkubwa kwa ajili ya maadhimisho hayo Alhamisi (Juni 30) , wakipeperusha bendera na kutazama picha kubwa ya Lumumba.

Lumumba aliuawa kwa kupigwa risasi Januari 16, 1961, kusini-mashariki mwa jimbo la Katanga baada ya kuondolewa madarakani kama Waziri Mkuu mwaka 1960 ndani ya miezi kadhaa baada ya DRC kupata uhuru kutoka kwa Ubelgiji.

Bango lenye maneno "shukrani nyingi, Shujaa wa Kitaifa" lilisimamishwa juu ya umati wa watu, akiwamo Rais wa Jamhuri ya Congo, jirani, Denis Sassou Nguesso, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ubelgiji na mabalozi kadhaa wa Afrika.

"Hatimaye watu wa Kongo wametoa heshima na kufanya mazishi kwa waziri mkuu wao mashuhuri," anasema Rais Felix Tshisekedi na kuongeza. "Tunamaliza ... maombolezo tuliyoanza miaka 61 iliyopita"

Baada ya mazishi hayo ni kuwa ambacho hakipingiki ni ukweli kuwa Congo kupata uhuru kuliitumbukiza katika dhahma ambayo imedumu muda wote huo mpaka sasa.

Kulianza na kuuawa kwa kiongozi wa harakati za uhuru Waziri Mkuu Patrice Lumumba na mwili wake unadaiwa kuyeyushwa katika tindikali na mabaki kuhifadhiwa Ubelgiji na sasa jino lake la dhahabu lilirudishwa na kuzikwa nchini humo.

Kwa nchi kama Tanzania, haikuwa na mapito ya kutisha kama majirani Kenya, Zambia ambako kulikuwapo msukosuko kiasi chake.

Ila kwa upande wa Zanzibar,inafanana na Rwanda na kwa mbali Uganda, kuwa siku ya uhuru ni mapinduzi, ambako mifumo kandamizi ya jadi iliyoheshimiwa na kulindwa na utawala wa kikoloni iliondolewa kwa kumwaga damu.

> Nchini Uganda uhuru ulileta kazi moja ya kumwondoa Kabaka wa Buganda kama Rais wa nchi; huko Zanzibar uhuru ulimwondoa Sultani aliyeachwa upweke na Waingereza akapinduliwa ndani ya siku 40.



Lumumba

Nchini Uganda uhuru ulileta kazi moja ya kumwondoa Kabaka wa Buganda kama Rais wa nchi; huko Zanzibar uhuru ulimwondoa Sultani aliyeachwa upweke na Waingereza akapinduliwa ndani ya siku 40.

Ambacho kinaonekana wazi, ni kwamba Afrika kupata uhuru halikuwa jambo lililoleta faida ya wazi kwa nchi za Afrika.

Uhuru uliendana na hisia za nchi za Afrika, za wasomi wao na wananchi waliohamasishwa, licha ya kuwa baadhi ya watiifu wa wakoloni nyakati hizo walichelea kuondoka kwa Wazungu, halafu Waafrika waanze kutii mtu mwingine ambaye siyo mkoloni ilikuwa ngumu.

Wengi katika nchi hizo walishindwa mtihani huo, kwani uhuru ulikuwa unahitaji imani, yaani utii bila ya woga uliotangulia kama ule wa kuiogopa serikali ya kikoloni chini ya gavana na polisi wa mzungu.

Tofauti na imani kama hiyo, uhuru ulipohakikishwa kila kundi la kisiasa au kijamii likaweka maslahi yake mbele kwa vile yasingeweza kufikiwa kama yalivyoahidiwa, haikuchukua muda kwa mitafaruku kuanza kuonekana katika baadhi ya mataifa.

Njia rahisi zaidi ya kuunganika kisiasa kwa maslahi ya makundi na siyo taifa kwa jumla ilikuwa ni kuendeleza ukabila katika harakati hizo za awali, kabila lililoweza kudhibiti jeshi likawa ndilo linalotawala.

Tatizo hilo lilianza kuonekana mapema licha ya kuwa dalili hizo hazikuondoa imani kwa umuhimu wa uhuru wenyewe, na baadaye ikazuka dhana ya 'ukoloni mamboleo', kuwa wakoloni wameondoka, ila wanatawala kupitia milango mingine.

Hiyo ilichukua sura, iwe ni kisiasa kwa kutumia 'vibaraka' au ni ya kiuchumi kwa kumiliki njia muhimu za uchumi kama sekta za madini, benki na bima.

Ila waliojitahidi kupambana na hali hiyo kwa kutaifisha mali hizo, pia walijizuia uwekezaji, tumaini lao likawa kuuza mazao nje na kuweka msingi wa viwanda lakini wengi wakakwama.

Kimsingi, ndiyo hapo Afrika imefikia baada ya miaka 61 licha ya kuwa ishara za hali hiyo na mijadala kuhusiana na majanga yake zimekuwepo miaka yote.

Kielelezo ni kuuawa kwa Rais Sylvanus Olympio wa Togo Januari 1963, mwaka mmoja baada ya Tanganyika kuwa jamhuri, na Rais Julius Nyerere akatambua kuwa hali hiyo ni ya hatari kwa viongozi wote (wa kiraia) katika nchi huru za Afrika.

Ni hali iliyochochea kuundwa kwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) Mei 1963, na viongozi kama Rais Dk.Kwame Nkrumah wa Ghana kusisitiza Afrika kuungana kisiasa kuwa nchi moja ili zisichezewe na 'mabeberu.'

Ukweli ni kwamba ukoloni ulitumia mianya ya ukabila na kujinufaisha miongoni mwa wakuu wa nchi hizi, au kuwalipa 'vijisenti' wakuu wa jeshi (wenye dhamira ya kuongoza na kujinufaisha na ambao pia ni wakabila.

Kwa lugha ya Mwalimu Julius Nyerere, wakoloni waliona kuna haja ya kuwaondoa viongozi 'wakorofi' madarakani, wanaoingilia milki zao za kiuchumi.



# Wenye leseni za uchimbaji watahadharishwa

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WAZIRI wa Madini Dotto Biteko, ameagiza watu wote waliopewa leseni za uchimbaji madini na hawafanyi shughuli za uchimbaji kufutiwa umiliki wao kwa mujibu wa sheria ya madini inavyoelekeza.

Biteko, alibainisha hayo juzi wakati wa ziara yake ya kukagua mgodi wa uchimbaji chuma ghafi katika Kijiji cha Asanje, wilayani Bahi, mkoani Dodoma.

Alisema, wachimbaji wa madini wote waliopatiwa leseni na wizara yake wanapaswa kufanya shughuli za uchimbaji kwa wakati kama sheria inavyoelekeza.

"Wachimbaji wote wa madini pamoja na madini yanayotumika viwandani wanapaswa kufanya shughuli ndani ya muda ulioelekezwa kwa mujibu wa sheria na atakaye kwenda kinyume afutiwe leseni.

"Wenye leseni kubwa za uchimbaji sheria inalekeza kuanza kufanya kazi ndani ya miezi 18 na wenye leseni ndogo ni miezi mitatu kama atakua hajaanza uchimbaji anafutiwa leseni yake," alisisitiza Biteko.

Alisema hali hiyo itasaidia kupunguza madalali wanaokata leseni na kushikilia maeneo bila kuwa na uwezo wa kuchimba madini.

"Wengi ambao wamekuwa wakimiliki leseni ni madalali wanamiiliki, lakini hawana uwezo wa kuchimba hivyo wote ambao watashindwa kutekeleza sheria ya madini hatua zichukuliwe dhidi yao," alisema.

Aliagiza wenye leseni wote kuweka mpango wa kuhudumia jamii ili kunufaika na rasilimali hiyo.

"Lazima kuwapo na mpango wa CSR wa kuhudumia jamii wateendeni haki watu waliopo katika maeneo ya migodi kwa kufanya shughuli za kusadia jamii kama vile ujenzi wa hospitali, shule na huduma nyingine," alisema. Kadhalika, aliwataka wachimbaji madini kuwa na umoja wenye nguvu ili kupambania haki zao ikiwamo bei elekezi za madini yao.

Mwenyekiti wa wachimba chuma ghafi, Peter Rweikila, alisema moja ya changamoto wanayokumbana nayo ni wenye viwanda vinavyohitaji malighafi hiyo kununua kwa bei ya chini.

"Mheshimiwa waziri wenye viwanda bado wananunua malighafi hii kwa bei ya chini ukilinganisha na bei elekezi iliyowekwa na serikali," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alimuomba waziri huyo kuwasaidaia wakazi wa kijiji hicho kunufaika na uwapo wa madini hayo.

Mnkunda, alisema pamoja na uwapo wa mgodi huo bado hawanufaiki kutokana na wawekezaji kutowalipa baada ya kufanya kazi.

"Waziri kuna watu wana malalamiko ya kutolipwa toka mwaka jana, lakini pia kiasi wanacholipwa ni kidogo sana ambacho ni Sh. 250 kwa ndoo moja ya mawe yenye madini chuma," alisema.

## Serikali yaombwa kupunguza masharti mikopo kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kupunguza masharti ya mikopo kwenye Benki ya Kilimo ili wakulima wa zao la pareto ambao kwa asilimia kubwa ni wazee wanufaike nayo.

Mwenyekiti wa wadau wa zao hilo, Anangisye Sanga, alitoa kauli hiyo kwenye mkutano wa mwaka wa Bodi ya zao hilo, uliofanyika jijini hapa.

Alisema wanaolima zao hilo ni wazee na serikali inapaswa kuliangalia suala la masharti ya mikopo ili nao wakopeshwe na kuendeleza zao hilo.

Sanga alisema lengo lao ni kuona zao hilo linasonga mbele katika maeneo ambayo linazalishwa hapa nchini.

Naye, Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Gidion Mapunda alisema mkutano huo unalengo la kujadiliana kero zinazowakabili ili zitafutiwe ufumbuzi.

Alisema malengo ya mkutano huo ni pamoja na kuonyesha dira na mipango ya namna ya uzalishaji wa zao la pareto nchini, ikiwa ni namna gani wanaweza kufanya ili wanunuzi na wasindikaji waongeze bei kwa wakulima.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Lucas Ghadyo, alisema wameazimia bei elekezi ya msimu wa zao la pareto kuwa ni Sh. 3,200 kwa kilo na kila msimu lazima kuwe na mabadiliko ya bei.

Alitaja kero zinazowakabili ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanachangia wakulima kupoteza mazao yao shambani.

Alisema kero nyingine ni kukosekana kwa sehemu ya kukaushia pareto na nyingine kupungua kiwango kutokana na kutokauka.

Alisema kutokana na hali hiyo serikali kwa kushirikiana na Bodi hiyo wanakwenda kuwajengea vikaushio ili viwasaidie kukausha na kuepuka kupoteza maua.

Pia, alisema wanakwenda kutoa elimu kwa wakulima ili waache kulima kwa mazoea waendane na mabadiliko ya tabianchi.



Mwonekano wa mbele wa shule ya Sekondari ya Central ya jijini Dodoma, baada ya maduka yaliyojengwa shuleni hapo, kuvunjwa na uongozi wa Jiji hilo juzi, kwa madai kuwa yamejengwa bila kibali. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wanaokwepa kufanya usafi wa mazingira kukiona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa Kata za Jiji la Dodoma, wameagizwa kuwachukulia hatua za kisheria wananchi wanaokwepa kufanya usafi wa mazingira kwenye maeneo yao.

Mkuu wa Idara ya Mazingira na udhibiti taka ngumu wa jiji hilo, Dickson Kimaro, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa Mtaa wa Mwaja.

Alisema suala la usafi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja ili kulifanya Jiji la Dodoma kuwa na hadhi ya mazingira yaliyo mazuri.

Mkuu huyo alisema kuwa watu ambao hawataki kujitokeza kuungana na wenzao kufanya usafi na kuonekana kudharau watachukuliwa hatua za kinidhamu pamoja na kutozwa faini.

"Katika suala la usafi haliangalii mtu kwa cheo chake, kazi yake wala uwezo wake kinachotakiwa ni watu wote kujitokeza kufanya kazi."

"Nimesikia kuwa kuna watu wanajifungia kwenye nyumba zao hususani wenye nyumba zenye mageti hawajitokezi kushirikiana na wenzao katika kufanya usafi wakati suala hili ni la kila mmoja wetu."

"Kutokana na tabia hiyo nawaagiza watendaji na wenyeviti wa mitaa wote kuhakikisha mnawachukulia hatua za kisheria wale wote ambao hawajitokezi katika shughuli za kufanya usafi," aliagiza Kimaro.

Alihimiza wananchi wa jiji hilo kupanda miti ya matunda na kivuli.

Naye, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwaja, Athumani Mkuka, aliwataka wakazi wa mtaa huo kufanya usafi wa mazingira yao kila siku na kila wakati.

Alikumbusha usafi uwe sehemu ya maisha yao badala ya kusubiri kusukumwa na viongozi wa kiserikali.





# Kampuni yachangia mifuko 1,000 saruji ujenzi wa shule

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

KAMPUNI mpya ya ununuzi wa tumbaku ya Amy Holding Company Limited, imeahidi kuchangia mifuko 1,000 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Wasichana ya Mayeka, inayojengwa kwenye Kata ya Lupa, Tingatinga wilayani Chunya.

Kampuni hiyo imeahidi kushiriki pia kwenye ununuzi wa madawati wa shule hiyo inayotarajiwa kufunguliwa mwezi Januari, mwakani.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Ahmed Howel, alitoa ahadi hiyo wakati Serikali ya Mkoa wa Mbeya ilipokuwa ikiitambulisha kampuni hiyo kwa wakulima wa tumbaku katika wilaya hiyo.

Alisema mbali na michango hiyo pia ataendelea kushirikiana na serikali kwa kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo kupitia utaratibu wa kuchangia huduma za jamii na kwamba walianza kuchangia shughuli hizo muda mrefu.

"Sisi kwa kuanzia tutachangia mifuko 1,000 ya saruji kwa ajili ya mradi huu na tutashiriki pia kwenye ununuzi wa madawati kwa ajili ya wanafunzi madarasa yatakapokuwa yamekamilika," alisema Howel.

Awali, akizungumza kwenye mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, ambaye shule hiyo imepewa jina lake, aliwaomba wadau mbalimbali wa maendeleo kushirikiana na serikali kwenye ujenzi wa mradi huo.

Alisema katika wilaya hiyo hakuna shule yoyote ya wasichana hali ambayo inawafanya wengi kushindwa kumaliza masomo kutokana na matatizo mbalimbali ya kimazingira.

Alisema wasichana wengi wa wilaya hiyo wanakatisha masomo kutokana na kupata mimba wanapokuwa shuleni, anaamini kuwa shule hiyo itakuwa mkombozi kwa kundi hilo.

Baada ya wazo la ujenzi wa shule hiyo kuanzishwa, walishirikiana na viongozi wa vijiji na Kata ya Lupa Tingatinga kutafuta eneo ambalo walilipata na kuanza ujenzi haraka.

"Tunawashukuru wadau ambao wanaendelea kujitokeza kuchangia ujenzi wa shule yetu, tunaamini kwamba mpaka kufikia mwezi Januari, itakuwa imekamilika, itakuwa ni shule ya bweni kwa hiyo tunahitaji michango ya wadau kwenye ujenzi wa mabweni," alisema Mayeka na kuongeza.

"Hii shule ndiyo itakuwa suluhisho la tatizo la mimba maana mazingira yetu ni ya mapori ambayo wasichana wakitembea umbali mrefu ni rahisi kukumbana na vishawishi," aliongeza Mayeka.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alikemea baadhi ya wanaume wanaowarubuni watoto wa shule na kuwatia mimba na kuonya atakayepatikana atachukuliwa hatua kali za kisheri ikiwamo kupelekwa mahakamani.

Homera alisema baadhi ya mafataki wanatumia fedha zao kuwarubuni watoto wa kike na kufanya nao mapenzi hali ambayo huwasababishia mimba.

Homera alisema kutokana na hali hiyo aliamua kuanzisha wazo la ujenzi wa shule hiyo ili kuokoa kundi la watoto wa kike wanaokatisha masomo.

Chunya ni miongoni mwa wilaya zinazokabiliwa na tatizo kubwa la wanafunzi kukatisha masomo kwa kupata mimba.




Mstaafu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Stephen Mwakajumilo (kushoto), akipokea fomu ya kuwania Uenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kutoka kwa Katibu wa Chama hicho Mkoa, Mwalimu Shaib Akwilapo katika ofisi za chama hicho, jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Rais Samia anatarajiwa mgeni rasmi Nanenane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha Maonyesho ya Wakulima (Nanenane), kitaifa ambayo yatafanyika mkoani Mbeya Agosti 8, mwaka huu.

Maonyesho hayo yanatarajiwa kuzinduliwa rasmi Agosti mosi, mwaka huu na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na kwa mara ya kwanza yatashirikisha wageni kutoka katika mataifa nane yanayopakana na Tanzania.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maonyesho hayo ambayo yanafanywa kwa ushirikiano wa mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini.

Homera alisema maandalizi ya Uwanja wa John Mwakangale, utakaotumika kwenye maonyesho hayo yamefikia zaidi ya asilimia 88 na baada ya wiki moja yatakuwa yamefikia asilimia 92, kabla ya Agosti mosi, yatakuwa yamekamilika.

Alisema maonyesho hayo ni ya kipekee akisisitiza kuwa yamepelekwa katika kanda hiyo kutokana na upekee wake kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara.

"Mikoa yetu ya Nyanda za Juu Kusini ndiyo ghala la chakula kwa taifa letu kutokana na kuwa vinara kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali na hivyo maonyesho haya yatatusaidia kutathmini namna ambavyo wakulima wetu wamejifunza," alisema Homera.

Pia alisema Mkoa wa Mbeya unaendelea na mikakati mbalimbali ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati ikiwamo soya zao ambalo Tanzania imepata soko nchini China.

Alisema mpaka sasa sekretarieti ya maandalizi imeshaanza kugawa viwanja kwa wadau wa maonyesho kwa ajili ya kuweka mabanda ya kufanyia shughuli zao. Aliwataka wananchi wote nchini ambao wanataka kushiriki kwenye maonyesho hayo kuwahi kuomba viwanja ili wapate mapema na kujenga mabanda.

Alisisitiza maonyesho ya mwaka huu yatakuwa tofauti na miaka mingine kutokana na kuandaliwa utaratibu mzuri wa watu kuingia uwanjani ili kuepuka misongamano isiyokuwa ya lazima kwenye mageti.

# Wakulima mpunga wataka udhibiti vipimo 'lumbesa'

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga wilayani Mbarali, wameiomba serikali kuwadhibiti wanunuzi wa zao hilo wanaotumia vipimo visivyoruhusiwa ikiwamo ujazo mkubwa ujulikanao kama 'lumbesa'.

Waliiomba serikali kuwalazimisha wanunuzi wote wa zao hilo kununua kwa kutumia mizani badala ya kupima kwenye madebe na mifuko yenye ujazo usiojulikana ili kuepuka unyonyaji unaowasababishia hasara.

Ombi hilo lilitolewa wakati wa utoaji wa elimu ya kilimo bora cha mpunga iliyotolewa na kampuni ya usambazaji wa mbolea ya YARA Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), kituo cha Uyole.

Elimu hiyo ilitolewa katika shamba darasa lililoandaliwa na taasisi hizo katika Skimu ya Umwagiliaji ya Matebete iliyoko katika Kata ya Chimala, wilayani humo na wakulima hao kulalamika kupata hasara.

Mmoja wa wakulima hao, Edward Mwakifwamba, alisema baadhi ya wakulima wananunua mazao hayo kwa kushindilia kwenye mifuko ambayo ujazo wake haujulikani.

Alisema kitendo hicho kina wasababishia hasara wakulima kutokana na kupata kipato kisichoendana na gharama za uzalishaji wa zao hilo.

"Tunataka tusaidiwe kuuza mazao yetu kwa kutumia mizani, sisi hata tukiuza kilo moja kwa Sh. 1,000 tunaamini tutapata faida nzuri na tutapata tija kwenye zao hili, lakini sio sasa hivi wanunuzi wanakuja na mifuko yao," alisema Mwakifwamba.

Akiwa ziarani mkoani Mbeya mwaka juzi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipiga marufuku wanunuzi wa mazao ya wakulima kutumia ujazo wa lumbesa huku akiwataka viongozi wa serikali kusimamia utekelezaji wa katazo hilo.

**Alisema kitendo hicho kina wasababishia hasara wakulima kutokana na kupata kipato kisichoendana na gharama za uzalishaji wa zao hilo.**



## Dk. Mwinyi amulika uwajibikaji watendaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amewataka watendaji wa wizara za serikali kufanya kazi kwa bidii, ushirikiano na kuaminiana ili kuwatumikia Wazanzibar ipasavyo.

Dk. Mwinyi alihimiza hayo jana katika hafla ya kuwaapisha Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar aliowateua Juni 30 mwaka huu.

Alisema pamoja na mambo mengine, uteuzi wa watendaji hao umezingatia sababu kuu mbili, ikiwamo baadhi ya watendaji wa wizara hizo kufanya kazi bila maelewano na hivyo kukosekana ufanisi.

Rais alisema amewarejesha Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara za Serikali ya Awamu ya Saba kuendelea na nyadhifa hizo kwa lengo la kuwaongezea nguvu makatibu wakuu kutokana na kuzidiwa na majukumu sambamba na kazi kutetereka pale watendaji hao wanapokuwa hawapo.

"Hakukuwa na sababu ya kuteua watendaji wapya, ni matarajio yangu hawa waliokuwa katika awamu ya saba watatenda vyema," alisema.

Aliwataka watendaji hao kufanya kazi kwa bidii na kuahidi kuwapandisha vyeo watendaji wote watakaotekeleza vyema majukumu yao ya kazi.

Baadhi ya ofisi na wizara za serikali ikiwamo Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, hazikufikiwa na mabadiliko na uteuzi huo.

Taasisi zingine ambazo hazikufikiwa na mabadailiko na uteuzi huo ni Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Katika hafla hiyo, viongozi mbalimbali wa kitaifa walihudhuria, akiwamo Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Mwinyi Talib Haji, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmeid Said.

# Taasisi ya Mkapa yapongezwa mapambano dhidi ya UVIKO-19

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI imeupongeza Wakfu wa Mkapa (Benjamini Mkapa Foundation) kwa kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya UVIKO-19 na uboreshaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari kuelekea kumbukizi ya mwasisi wa taasisi hiyo, Benjamin Mkapa, Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Ali Nyange, alisema taasisi hiyo imeajiri wafanyakazi wa afya 105 wanaotoa huduma hospitali na vituo vya afya 45 Unguja na Pemba.

Alisema hatua hiyo imesaidia kupunguza tatizo la uhaba wa wataalamu ambapo taasisi hiyo ndiyo inalipa mishahara ya wataalamu hao na kuongeza kasi ya upatikanaji huduma za afya.

"Hawa wataalamu 105 wakiwamo madaktari, wauguzi, watu wa maabara na wengine wanalipwa mishahara yao na Mkapa Foundation, kwa kweli taasisi hii imetusaidia sana katika kurahisisha kutoa huduma za afya kwa wananchi," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alisema taasisi hiyo imesaidia katika mapambano ya UVIKO-19, hasa katika kutoa elimu kwa wananchi kuchanja chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo na sasa watu waliochanjwa Zanzibar wamefikia 185,000, sawa na asilimia 30 ya malengo.

Alieleza kuwa ili Zanzibar iwe vizuri ni lazima wananchi wake walindwe dhidi ya maradhi mbalimbali ikiwamo UVIKO-19.

Dk. Nyange alisema licha ya mafanikio hayo, bado walio wengi hawajafikiwa hasa maeneo ya vijijini kwa sababu baadhi ya watu wanaamini chanjo hizo zinaweza kuwa na athari lakini kwa wote waliochanja, hakuna aliyepata tatizo.

"Baadhi ya watu wanazihusisha chanjo za UVIKO-19 na mfumo wa uzazi na mambo mengine ambayo hayana ukweli, niwasisitize wananchi waendelee kuchanja," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema chanjo ya UVIKO-19 ni sehemu ya utaratibu mpya wa dunia kwa sababu watu wote waliokwenda kuchanja walipata chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo.

Daktari wa Hospitali ya Wilaya Makunduchi, Dk. Mohammed Mnyimbi, alisema hospitali hiyo imepata mgawo wa wafanyakazi watano kutoka Mkapa Foundation ambao wamesadia uharakishaji wa utoaji huduma zinazotolewa hospitalini hako kwa wananchi.

"Wafanyakazi hao wakiwamo madaktari na wauguzi wamekuja muda mwafaka wakati ambao nchi inakabiliana na UVIKO-19, tulikuwa tumeelemewa na mzigo mkubwa wa utoaji huduma lakini pia Mkapa Foundation imesaidia kuongeza idadi ya wananchi waliopatiwa chanjo ya UVIKO-19 hospitalini hapa," alisema.

Alibainisha kuwa awali watu waliopata chanjo hospitali huko ni 300, lakini hivi sasa wamechanja watu 3,400 na kwa wilaya nzima ya Kusini Unguja waliopata chanjo ni 8,642 ambapo kwa Zanzibar ni wilaya ya pili iliyofanya vizuri kuchanja watu wengi.

Meneja wa Mkapa Foundation Zanzibar, Khadija Kassim, alisema taasisi hiyo inafanya kazi na Serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa huduma bora za afya na imeajiri wafanyakazi 105 ambao wanatoa huduma za afya Zanzibar na kuleta ufanisi katika utoaji huduma.

"Taasisi hii imefanya juhudi ya kuongeza wafanyakazi wa afya kutokana na uhaba mkubwa wa wafanyakazi hasa kipindi cha mripuko wa UVIKO-19 ili kuleta ufanisi katika kutoa huduma," alisema.




Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya wa Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Ali Nyange, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Zanzibar jana, kuhusu Taasisi ya Mkapa Foundation, ilivyoboresha huduma za afya kisiwani humo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Rais asifu ongezeko taasisi elimu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema kuongezeka kwa taasisi za elimu na ujuzi nchini kutasaidia kuongeza fani na taaluma kwa wananchi.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa uwekaji jiwe la msingi la ujenzi wa kituo cha ufundi kwa wanafunzi wa kike huko Bungi, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia kupunguza hali ya utegemezi kwa kuwajengea misingi bora wananchi, ikiwamo kujiajiri wenyewe.

Hemed alisema kumekuwa na taasisi nyingi zinazofanya kazi kwa lengo la kusaidia serikali katika sekta ya elimu, hivyo akawaomba wananchi kuthamini juhudi hizo na kuwa tayari katika kuona lengo hilo linafikiwa kwa kujitokeza kupata elimu na fani zitakazowasaidia kuwainua kiuchumi.

Aliipongeza Bodi ya MIF kwa kufanya kazi kwa kuzingatia mahitaji ya jamii kutokana na umuhimu wa elimu na kuonyesha kipaumbele zaidi kwa wasiokuwa na uwezo, watu wenye ulemavu na yatima.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation (MIF), Wanu Hafidh Ameir, alisema watahakikisha wanaitunza misaada hiyo ya kielimu wanayopatiwa na Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E) inayolenga kuwakomboa wananchi.

Akitoa salamu kutoka U.A.E, Sayyidah Maithaa Al Shaamy, alisema kukamilika kwa kituo hicho, kutasaidia kuwajengea uwezo wanafunzi wa kike katika kuwakuza kitaalamu na kubadilisha maisha yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

Nafasi za Kazi ya ualimu, sifa **Diploma au Digrii** masomo ya hesabu na science darasa la 6 na 7 Piga simu kabla ya tarehe 7/7/2022.

**Simu 0783298900**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**KIVUKONI/KINONDONI**
**RUFAA YA MADAI NAMBA: 139 YA 2022**
**RAPHAEL WALIANA KAUNDA..........................MRUFANI**
**BAINA YA RHOBI WAMBURA GIKARO.............................MRUFANIWA**

**KWA**
**RHOBI WAMBURA GIKARO.**
**DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mrufani ameleta rufaa yake ambayo maelekezo ya rufaa yameelekezwa katika nakala za rufaa ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ya mkoa, binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa kabla au siku ya Tarehe 13 Mwezi Saba (7) Mwaka 2022, saa 08:00 Asubuhi

Kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na rufaa hii.

**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo Tarehe 30 Mwezi June Mwaka 2022**

RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT
Hakimu Mkazi Mfawidhi
Mahakama ya Hakimu Mkazi kivukoni/Kinondoni

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BW. EZEKIEL MATHIASY NZOWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA** yenye usajili namba **T295BKD** yenye majina ya **ELIZABETH MEINRAD THINDWA** mnano tarehe **08/06/2021** maeneo ya Kijitonyama, Dar es Salaam. Kwa yeyote atakayeiona anaombwa kuwasiliana na mhusika kwa namba 0755522307 au kutoa taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/568308/2021**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN THOMAS LUGENGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3519-0070 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya KIVUKONI mwaka 2011,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa: IFA/RB/4339/2015**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**MARIA JOSEPHAT KIARIRO** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S0209-0040** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **KOROGWE GIRLS SECONDARY mwaka 2015** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S1626-0512 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **MARIADO SECONDARY** mwaka 2019,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Polisi taarifa SEG/RB/104/2022**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**WEMA MSOKWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P 0108/0007** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **IFUNDA SECONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka **1998.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa: **DSM/PHQ/RB/265902/2022**

---

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No.91 of 2022**
In the matter of the Estate of the late
**EDWARD ISACKA IRAMBA**
**And**
In the matter of an application for letters of administration by
**SHEDRACK EDWARD IRAMBA.**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 1 Day of 08,2022

**Dated at Dodoma this 01 day of 07,2022**

SHEDLACK
PETITIONER

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRIC
RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASIMWE JUSTAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index **No. S3627-0003** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **MAGNUS SECONDARY SCHOOL mwaka 2013.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/260133/2022.**

---

**RE: THE LAND ACT NO 4 OF 1999**
**LOSS OF ORGINAL LETTER OF OFFER**
**LOSS OF ORGINAL LETTER OF OFFER OF;**
**REF;NO.MMC/LD/20800**
**REGISTERED OWNER: ADAM BAKARI CHAMILUNDA**
**LAND 34 BLOCK "M.2" LOCATION KIWANJA CHA NDEGE**
**APPLICANT: ADAM BAKARI CHAMILUNDA**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGNAL LETTER OF OFFER** to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a **REPLACEMENT OF THE ORGINAL OF OFFER** in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty days from the date of this publication.

The **ORGINAL LETTER OF OFFER** if found should be delivered to the office of the Municipal Director,Morogororo Municipality Council, **P.O.BOX 166 Morogoro.**

Issued by

**Valency . HK**
**For; MUNICIPAL DIRECTOR, MOROGORO**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 170/2021**
**Jina la Mdai:SALIM KIMARO**
**Jina la Mdaiwa ALEX SHIGEMO.**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ALEX SHIGEMO WA NKUHUNGU DODOMA**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba (Eleza hapa habari za Madai) YA TSH. 350,000/-

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 06 Mwezi 07 Mwaka 2022 Saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila yaw ewe kuwepo

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 01 Mwezi 07 Mwaka 2022**

HAKIMU

---

**TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1485**

**POWERHOUSE AFRICA GROUP LIMITED**
**P.O. Box 60294**
**DAR ES SALAAM – TANZANIA**
**SPECIAL RESOLUTION**

At the Board of Directors meeting of **POWERHOUSE AFRICA GROUP LIMITED** held at the registered office, **POWERHOUSE AFRICA GROUP LIMITED** on the 1st **March, 2022,** the following resolutions were duly passed.

- To wind up the Company voluntarily in accordance with section 333(1) of the Companies Act **No. 12 of 2002.**
- The Company confirms that there are no reasons to prevent the dissolution of the Company.
- RSG Attorneys has been appointed as the liquidator for the purpose of winding up of the Company.

**Certified true copy:**

**Danford Paul Nchembi**
Director
Date 01/03/2022

**Shally Williard Mgalla**
Director
Date 01/03/2022

**Johnpaul thadei**
Company Secretary
Date 01/03/2022

---

## TANGAZO KUFUNGA KAMPUNI

TUNATANGAZA KUFUNGA KAMPUNI YA FAWAZ INTERNATIONAL COMPANY LIMITED YENYE CERTIFICATE OF INCORPORATION NO.141195BRELA NA TIN NO.135-902-276.
KIKAO CHA WAKURUGENZI KILIKAA TAREHE04/07/2022 NA KILIAZIMIA KUFUNGA KAMPUNI TAREHE 06/07/2022, KUTOKANA NA KUKOSA MTAJI WA KUENDESHA KAMPUNI.
**KWA MAELEZO NA MADAI WASILIANA NA:0782340029**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya MAKOLE**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai /Ndoa Na.51/2022**
**Jina la Mdai .......GIDION JULIUS MWANIBINGO**
**Jina la Mdaiwa ......JOSEPHINE JOSAM MJEMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

(Kanuni ya 18 ya kanuni ya taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

**KWA. JOSEPHINE JOSAMU MJEMA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA TALAKA KUACHANA**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 14 mwezi 07 mwaka 2022 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shihidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 04 mwezi 07 mwaka 2022.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 4 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GODFREY SALAYA KIVUYO**
**AND IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION BY AUDILIA MANG'ANYA KIVUYO GODFREY SALAYA KIVUYO.**

**GENERAL CITATION**

*(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)*

**ALL PERSON** Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AHMED ATHUMANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye **USAJILI NAMBA: MC380 CHR, CHASSIS NAMBA: LBRSPJB57K9007296 na ENGINE NAMBA: 19902314.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: KOR/RB/592/2022**

---

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Putin aamuru vikosi kusonga mbele

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Vladimir Putin amemwamuru waziri wake wa ulinzi kuendelea na mashambulizi nchini Ukraine, baada ya nchi hiyo kuuteka mji wa Lysychansk.

Putin alionyeshwa kwenye runinga ya taifa hilo, akitoa wito kwa vikosi vilivyoko sehemu zingine kutekeleza malengo yao kulingana na mipango iliyoidhinishwa hapo awali.

Utekaji huo unamaanisha kuwa eneo lote la Luhansk, sasa liko mikononi mwa Russia. Hapo awali gavana wa eneo hilo la Ukraine, alisema mji huo ulisalimishwa ili Warussia wasiuharibu kwa makombora ya mbali.

Sehiy Haidai, alisema wanajeshi wa Ukraine wamehamia maeneo mapya yenye ngome. Kupoteza mji huo na kukabidhi udhibiti wa Luhansk kwa Warussia ilikuwa jambo chungu.

"Hii ni vita moja tu tumepoteza, lakini sio mapambano." Alisema Haidai.

Aidha, aliomba silaha zaidi kutoka Magharibi ili kukabiliana nguvu za Russia.

**Russia sasa imeongeza mashambulizi yake katika miji katika eneo jirani la Donetsk, huku maeneo yanayozunguka Sloviansk na barabara kati ya Lysychansk na Bakhmut yakilengwa.**

Katika mkutano na waziri wake wa ulinzi, Putin aliwapongeza wanajeshi wa Russia akisema walioshiriki mapigano hayo wanastahili kupumzika kwa sasa, huku wanajeshi wengine wakiendelea kupambana katika sehemu zingine nchini Ukraine. Ushindi huu ndio wa kwanza kuipelekea Russia kukaribia kuyafikia malengo yake tangu majeshi yake yaliposhindwa wakati yakijaribu kuuteka Mji Mkuu Kyiev.

Rais Volodymyr Zelensky ameahidi kwamba jeshi lake litarejea kuchukua tena mji wa Lysychansk baada ya kupata silaha za kisasa.

Russia sasa imeongeza mashambulizi yake katika miji katika eneo jirani la Donetsk, huku maeneo yanayozunguka Sloviansk na barabara kati ya Lysychansk na Bakhmut yakilengwa.

Mikoa ya Donetsk na Luhansk kwa pamoja huunda eneo la viwanda la Donbas.

**UJENZI WA RELI YA KUUNGANISHA RUSSIA NA UKRAINE**

Russia ina mpango wa kuanzisha ujenzi wa reli ambayo itaunganisha mji wake wa kusini wa Rostov na mingine ya mashariki mwa Ukraine ya Donetsk na Luhansk.

Habari hiyo ni kwa mujibu wa shirika la habari la TASS, likinukuu serikali ya mkoa wa Rostov.

Jumapili iliyopita Russia iliyaweka mazingira ya udhibiti kamili wa mkoa wa Luhansk na kwa sasa ipo katika mapigano makali yenye lengo la kuwaondoa kabisa wanajeshi wa Ukraine katika viunga vya mji wa Donetsk.

Wakati mapigano yakiendelea balozi wa Marekani nchini Ukraine, Bridget Brink amezuru katika kituo kimoja cha kijeshi mjini Kyiv, pamoja na mambo mengine ziara hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kumbukumbu ya Uhuru wa Marekani.

Alisema hawezi kutabiri ni lini vita hivyo alivyoita vya kikatili vitaisha, lakini anaweza kutabiri kwamba Ukraine itashinda.

**UJENZI MPYA WA UKRAINE NI WA MUDA MREFU**

Katika mkutano wa kimataifa wa kuweka mpango wa ujenzi mpya wa taifa hilo unaofanyika Uswisi, Waziri wa Maendeleo wa Ujerumani Svenja Schulze, alitahadharisha kutahitajika jitihada kubwa ya kuijenga upya Ukraine. Akizungumza na shirika la habari la Ujerumani DPA, Schulze alisema mradi huo si wa mwaka mmoja au miwili.

Katika mkutano huo ulioanza Jumatatu, Waziri Mkuu wa Ukraine, Danys Shmyhal alisema ujenzi wa miundombinu ya Ukraine utahitaji Euro bilioni 750.

Hata hivyo, waziri Schulze alisema hatua hiyo pia itatoa fursa kwa Ujerumani.

Kabla ya vita na watu wengine kulikimbia taifa hilo Ukraine ilikuwa na watu karibu milioni 44. **BBC**




Helikopta ikizima moto unaowaka katika msitu karibu na Kanisa la Katoliki la Mt. Peter Basilika kaskazini mwa mji wa Rome nchini Italia jana. **PICHA: REUTERS**

## Mtu aliyeua watu 6 akamatwa

**WASHINGTON,** Marekani

POLISI wa Marekani wamemkamata mshukiwa mmoja ambaye anahusishwa na tukio la kuwaua watu sita kwenye gwaride la Siku ya Uhuru karibu na Chicago.

Polisi wanasema Robert E Crimo III (pichani), mwenye umri wa miaka 22, alizuiliwa baada ya msako mfupi.



Takriban watu wengine 24 walijeruhiwa katika jiji la Highland Park, Illinois, baada ya mtu mwenye bunduki kuwalenga watu kutoka juu ya paa.

Ni ufyatuaji risasi wa hivi punde zaidi nchini Marekani.

Rais Joe Biden alisema alishtushwa na ghasia hizo.

Crimo alizuiliwa baada ya kufanyika msako mkali. Alitajwa kama mtu anayefaa kuhojiwa katika tukio la ufyatuaji risasi siku ya Jumatatu.

Hata hivyo, kukamatwa kwake polisi walisema waliamini kuwa alihusika.

Mtu mwenye bunduki alifyatua risasi kwenye gwaride mwendo wa saa 10:15 saa za ndani (15:15 GMT), dakika chache tu baada ya kuanza.

Hafla hiyo ilipangwa kujumuisha bendi za kuandamana, na burudani ya jamii kama sehemu ya sherehe za Siku ya Uhuru wa jiji hilo.

Lakini badala ya kuwa ya furaha, ilibadilika haraka na kuwa yenye hofu na majonzi. **BBC**

## Jeshi Sudan kukabidhi madaraka kwa raia

**KHARTOUM,** Sudan

KIONGOZI wa kijeshi wa Sudan ametangaza kuwa atalivunja baraza huru analoliongoza na kukabidhi madaraka kwa serikali mpya ya mpito.

Hata hivyo, Jenerali Abdel Fattah Burhan hakutoa ratiba kamili ya kipindi ambacho makabidhiano yatafanyika au jukumu ambalo jeshi litakuwa nalo katika muundo wa serikali uliopendekezwa.

Katika hotuba yake kwa njia ya televisheni, Jenerali Burhan pia alitangaza jeshi halitahusika tena katika mazungumzo ya kumaliza mzozo wa kisiasa nchini humo, huku nafasi yake katika mazungumzo ikichukuliwa na mashirika ya kiraia.

Hatua hiyo ni kubwa kwa kiongozi huyo kuonekana kulegeza kamba wakati maandamano ya kudai demokrasia na jeshi kuachilia madaraka yakishika kasi nchini humo.

Jeshi lilichukua mamlaka katika mapinduzi ya Oktoba mwaka jana, baada ya kupindua serikali ya kiraia ya Waziri Mkuu Abdalla Hamdok.

Tangu wakati huo, muungano wa madaktari ulisema zaidi ya watu 110 wameuawa katika maandamano ya kupinga mapinduzi.

Wiki iliyopita, watu 9 waliuawa na vikosi vya usalama wakati wa siku mbili za maandamano ambayo yamekuwa makubwa zaidi tangu jeshi lichukue mamlaka mnamo Oktoba 2021. **BBC**

## Viongozi DRC, Rwanda kukutana Angola

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi, leo atakutana na kiongozi mwenzake wa Rwanda, Paul Kagame nchini Angola kwa ajili ya mazungumzo.

Mkutano huo unafanyika wakati mivutano baina ya nchi hizo jirani inazidi kuongezeka. Taarifa ya mkutano huo imetolewa na msemaji wa serikali ya DRC, Patrick Muyaya ambaye amearifu kwamba Tshisekedi na Kagame watajadili uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo mbili na uasi unaoendelea mashariki mwa nchi hiyo.

Muyaya alisema viongozi hao watatafuta majibu ya kile amekitaja kuwa uchokozi wa Rwanda nchini DRC.

Moja ya ajenda zitakazojadiliwa ni madai kuwa serikali ya Rwanda inawaunga mkono wapiganaji wa kundi la M23. Hata hivyo Rwanda inakanusha. **DW**

# ZAWADI ZA NBC DODOMA MARATHON KUWEKA HISTORIA

**Na Mwandishi Wetu**

HAIJAWAHI kutokea! Ndivyo unavyoweza kuzielezea zawadi zitakazotolewa kwa washindi wa mbio za NBC Dodoma International Marathon zitakazofanyika Julai 31, mwaka huu jijini Dodoma, imefahamika.

Mbio hizo za kimataifa zitahusisha kilomita 42, kilomita 21 na kilomita 10 huku dhumuni likiwa ni kuchangia kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi.

Akitangaza zawadi za washindi, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Benki ya NBC, David Raymond, alisema maandalizi yamekamilika na zawadi zitakazotolewa zimelenga kutoa hamasa kwa wakimbiaji hasa wa ndani.

Raymond alisema mshindi wa kwanza katika mbio za kilomita 42 kwa upande wa wanaume na wanawake ataondoka na kitita cha Sh. milioni nane kila mmoja huku wapili akijitwalia Sh. milioni nne na watatu Sh. milioni mbili wakati wanne Shilingi milioni 1.5 na atakayekamilisha tano bora ataondoka na Sh. milioni moja.

"Kwa kuzingatia kuwa mcheza kwao hutunzwa, kwa Mtanzania ambaye atakuwa wa kwanza ataongezewa Sh. milioni mbili, kwa hiyo ataondoka na jumla ya Sh. milioni 10," alisema Raymond.

Kwa upande wa mbio za kilomita 21, mshindi wa kwanza atapata Sh. milioni nne ambapo Mtanzania atakayeshika nafasi hiyo ataongezewa Sh. milioni moja kama motisha na kufanya jumla ya zawadi kuwa Sh. milioni tano wakati mshindi wapili atapata Sh. milioni mbili, watatu Sh. milioni 1.5. wanne Sh. milioni moja wakati wa tano atajitwalia Sh. 700,000. Mbio za kilomita 10 mshindi atajipatia Sh. milioni 1.5 huku mshindi wa pili Sh. milioni moja na watatu Sh. 700,000, wanne Sh. 500,000 na watano atajishindia Sh. 300,000.


Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Benki ya NBC, Godwin Semunyu alisema mbio za mwaka huu zimelenga kutoa elimu ya saratani ambapo wameshirikiana na Taasisi ya Ocean Road ili kufanikisha zoezi hilo.

"Kikubwa katika zoezi hili ni kutengeneza utamaduni wa kupima mara kwa mara na sisi tunaamini kwa kutumia marathon hii tutapata jukwaa kubwa zaidi na tunaamini tutawafikia watu wengi zaidi," alisema ofisa huyo.

Aliongeza mbio hizo zitasaidia katika kufungua mipaka ya kibiashara kwenye mambo mbalimbali ikiwamo zao la zabibu ambapo wawekezaji watapata fursa ya kujionea uzalishaji wake na namna wanavyoweza kushirikiana na serikali katika kuongeza tija kwenye eneo hilo.

Katika harakati za kutoa elimu, kuweka kipaumbele cha afya na kuinua jamii, NBC marathon inatoa hamasa kwa wananchi wajitokeze na kujishindia zawadi ambazo zitawasaidia kuendesha majukumu ya kimaisha, kuwekeza katika biashara na kukuza mitaji mbalimbali.

Ili kujisajili kushiriki kwenye mbio hizi za kimataifa, unaweza kutembelea tovuti ya events.nbc.co.tz na kulipia ada ya Sh. 30,000 kwa mbio zote ambapo utajipatia vifaa vya kukimbilia ikiwamo jezi.




Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Benki ya NBC, Godwin Semunyu (wa kwanza kushoto) na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa NBC, David Raymond wakiwa kwenye picha ya pamoja wakati wa uzinduzi wa zawadi watakazokabidhiwa washindi wa mbio za Kimataifa za NBC Dodoma International Marathon 2022. Kulia ni mtangazaji wa kipindi cha Joto la Asubuhi, Gerland Hando pamoja na Mkurugenzi wa Uendeshaji wa EFM, Denis Busulwa. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mbeya Kwanza yatamba kurudi Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA timu yao ya kwanza kushuka daraja msimu huu, klabu ya Mbeya Kwanza imesema kuwa inakwenda kujipanga na wana imani msimu ujao watarejea tena kwenye Ligi Kuu kama ilivyokuwa kwa Ihefu.

Ofisa Mtandaji Mkuu wa klabu hiyo, Gideon Ngereza amesema pamoja na kushuka daraja, lakini wamejifunza mengi kwenye Ligi Kuu, hivyo wanakwenda kuyafanyia kazi ili hata wakifanikiwa kupanda tena msimu ujao wasiwe na matatizo.

"Ligi ilikuwa ngumu sana, tunakubali tumeshuka kihalali, lakini tuna uhakika wa kurejea tena kwenye Ligi Kuu msimu ujao wa 2023/24 kwa sababu tumejifunza mengi ambayo tulikuwa hatuyajui," alisema Ngereza.

Alisema moja ya vitu walivyojifunza ni kuwa na wachezaji wenye ubora na vitu hivyo walikuja kuvifanya kipindi cha dirisha dogo waliposajili wachezaji wengi wenye uwezo wa hali ya juu, lakini walikuwa wamechelewa.

"Ligi inahitaji vitu vingi ikiwamo wachezaji wenye ubora na uwezo mkubwa na kweli dirisha dogo tulifanya hivyo timu ikaimarika, lakini kuna mambo mengi yakapitika, wachezaji wetu tegemeo wakawa majeruhi, lakini pia kufungiwa kwa kocha wetu Mbwana Makata na msaidizi wake kulitusumbua sana. Kwa sasa tunakwenda kujipanga kucheza ligi ya Champioship, naamini kwa jinsi tulivyojipanga na tayari tumeshajua sababu ya sisi kushuka, tutarejea kwenye Ligi Kuu," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Mbeya Kwanza ilishuka daraja ikiwa na pointi 25, ikiburuza mkia kwa kucheza mechi 30, ikishinda tano, sare 10 na kupoteza mechi 15.

Wakati huo huo, Ngereza amesema wamepata maombi kutoka kwenye klabu mbalimbali zikitaka kuwachukua wachezaji wao. Alisema kutokana na kwamba mpira ni biashara na kwa sasa ni maisha ya wachezaji, alizitaka klabu zote zinazohitaji wachezaji wake ambao wako kwenye mkataba kufuata taratibu zinazotakiwa na hatomzuia mchezaji wake yeyote anayetaka kwenda popote, mradi tu taratibu zimefuata.

"Unakumbuka tulimruhusu Chrispin Ngushi kwenda Yanga kipindi cha dirisha dogo, kwa hiyo sisi hatuzuii mchezaji," alisema.

# Azam yafunga usajili wa wazawa

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukamilisha usajili wa Mshambuliaji wa Coastal Union, Abdul Seleman (Sopu), uongozi wa Azam FC umeweka wazi kwamba, wamefunga usajili kwa wachezaji wazawa huku wakihitaji nyota wawili wa kigeni kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania na Kombe la Shirikisho Afrika.

Azam imetambulisha wachezaji wawili kutoka nje ya Tanzania ambao ni Kipre Junior na Tape Edinho na mzawa wawili Cleophance Mkandala na Sopu aliyesaini juzi mkataba wa miaka mitatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema kuhusu usajili wa wachezaji wa ndani (wazawa) wamefunga na sasa wanahitaji kumaliza usajili kwa wachezaji wawili akiwamo beki na kipa kutoka nje.

Alisema mchakato wa kupata wachezaji hao unaendelea na wamedhamiria kusajili wachezaji mahiri ili kufikia malengo yao ya msimu ujao kufanya vizuri katika ligi na michuano iliyopo mbele yao.

"Ni kweli tumekamilisha usajili wa wachezaji wazawa na sasa tunaangalia wachezaji wawili akiwamo kipa na beki kutoka nje ya Tanzania baada ya hapo tunafanya usajili wetu na kujiandaa na maandalizi ya msimu ujao," alisema Popat.

Alisema msimu uliopita hawakufanya vizuri na imekuwa funzo kwao na kuimarisha zaidi kikosi cha timu hiyo kwa kuhakikisha msimu ujao wanakuwa vizuri na kufikia malengo yao.

# Bondia Mandonga apania kumchapa Bondia Kaoneka

**Na Saada Akida**

BONDIA Karimu Mandonga atashuka ulingoni kuzichapa na Shabani Kaoneka katika pambano la uzito wa kg 76, linalotarajiwa kuchezwa Julai 30, mwaka huu.

Mabondia hao watapanda ulingoni wakisindikiza pambano la 'Payback Night' usiku wa deni kati ya bondia wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania 'JWTZ', Seleman Kidunda dhidi ya Tshimanga Katompa, litakalofanyika Uwanja wa Majimaji Songea, Ruvuma.

Mandoga anahitaji kulipa kisasi baada ya kukubali kichapo cha KO raundi ya Kwanza dhidi ya Kaoneka katika pambano lililopita la Twaha Kiduku dhidi ya Alex Kabangu, la kuwania mkanda wa UBO, lililofanyika Machi mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mandonga alisema wamejipanga vizuri kwenda kulipa kisasi kwa Kaoneka katika pambano hilo litakalofanyika Songea.

Alisema anaendelea na maandalizi kwa ajili ya kuhakikisha analipa kisasi kwa mpinzani wake huyo katika usiku huo wa kisasi dhidi ya Kaoneka.

"Pambano la Kaoneka nimekubali niliishia njiani lakini sasa nimefanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya kuhakikisha namchapa mpinzani wangu," alisema Mandonga.

Mbali na pambano hilo kutakuwa na mapambano mengine ya utangulizi ambayo wakimsindikiza Kidunda ambaye naye amedhamiria kufanya kweli kwa kumchapa Tshimanga Katompa.

## ZISIKUPITE

### RONALDO ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wanafikiria kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo, ambaye amewaarifu mashetani wekundu hao kuwa anataka kuondoka msimu huu wa joto. ***(Athletic)***

### CHELSEA NA OFA

CRISTIANO Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, anaweza kuwa tayari kujiunga na Chelsea, lakini The Blues hao bado hawajaamua kutoa ofa rasmi kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno. ***(ESPN)***

### RONALDO KUREJEA LALIGA

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta na wakala, Jorge Mendes pia wanajadili uwezekano wa nyota wa zamani wa Real Madrid Cristiano Ronaldo kurejea LaLiga. ***(AS)***

### STERLING AKARIBIA KUONDOKA

CHELSEA ipo kwenye mazungumzo ya juu na Manchester City kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27, ambaye thamani yake inakadiriwa kuwa pauni milioni 50. ***(Sky Sports)***

### ZIYECH HUYO MILAN

AC Milan wanashughulikia mpango wa kumsajili winga wa Chelsea kutoka Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29 kwa mkopo. ***(Athletic)***

### MARTINEZ NA MAN

MAOFISA wa Manchester United walikutana na wenzao wa Ajax wikendi kujadili kuhusu kumnunua mlinzi wa kimataifa wa Argentina, Lisandro Martinez mwenye umri wa miaka 24, huku mashetani hao wekundu wakitoa pauni milioni 39.6. ***(Mirror)***

### DEPAY HUYO SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imefanya uchunguzi kumnunua mshambuliaji wa kimataifa wa Uholanzi na Barcelona, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28, ambaye anaweza kuondoka pale Nou Camp kwa pauni milioni 17. ***(Sport)***

### BROJA AGOMBEWA

KLABU ya Everton na West Ham zote zinawania kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20 kutoka Chelsea, huku mshambuliaji huyo akiwa na thamani ya pauni milioni 30. ***(Mail)***

### TAGLIAFICO KUTUA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inataka kumsajili mlinzi wa kushoto wa Argentina, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 29, ambaye anapatikana kutoka Ajax kwa ada ya pauni milioni 3.3 pekee. ***(Sussex Live)***

### DIABY HUYO NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle bado ina nia ya kumsajili winga wa kimataifa wa Ufaransa, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 22 kutoka Bayer Leverkusen. ***(Sky Sports)***

### SINISTERRA KUTUA LEEDS

KLABU ya Leeds United ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili winga wa Colombia, Luis Sinisterra mwenye umri wa miaka 23 kutoka Feyenoord. ***(Express)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN U YAPAMBANA KUMBAKIZA RONALDO

## Hajaripoti mazoezi hadi sasa, akitaka...

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imesisitiza kuwa itapambana kumbakisha Cristiano Ronaldo katika klabu hiyo kwa muda uliosalia wa mkataba wake licha ya mchezaji huyo kutaka kuondoka, kwa mujibu wa 90min.

Ronaldo ameweka wazi kwa United hivi karibuni kwamba, anatamani kupewa nafasi ya kuondoka Old Trafford mwaka mmoja baada ya kurejea ikiwa ofa inayofaa itatolewa, na msimamo wake umewashangaza klabu na kocha mpya, Erik ten Hag.

Ten Hag - na hata Ronaldo mwenyewe mwezi uliopita - wote walikiri kwamba, wanasubiri kwa furaha kufanya kazi pamoja baada ya Mholanzi huyo kutua hapo kutoka Ajax.

**Lakini Ronaldo hana imani kwamba, United iko kwenye nafasi ya kuwania mataji makubwa na akiwa na umri wa miaka 37, angependa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka iliyosalia ya soka lake barani Ulaya.**

United hawajafurahishwa na hali hiyo na hawaoneshi dalili zozote kama wanataka kumuachia kwa sasa.

Klabu hiyo ina mpango wa kumbakisha na itapanga Ten Hag na Ronaldo kufanya mazungumzo kuhusu mipango ya baadaye.

Wawili hao bado hawajakutana ana kwa ana, hata hivyo, Ronaldo ndiye mchezaji pekee wa kikosi kizima cha United ambaye bado hajaripoti kwa mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya kule Carrington.

Ronaldo ameomba udhuru kwa sababu za kifamilia na hatakuwepo wiki yote hii - na shaka inaongezeka juu ya uwepo wake katika ziara ya kujiandaa na msimu wa klabu nchini Thailand na Australia na United inaondoka Ijumaa.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,012,7

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 7-9 JUNI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/07/22 | 13:00 | Kashiwa Reysol vs Nagoya Grampus | 2.35 | 2.94 | 2.99 |
| 02. 06/07/22 | 13:00 | Renofa Yamaguchi vs Oita Trinita | 3.15 | 3.05 | 2.20 |
| 03. 06/07/22 | 13:00 | Yokohama F Marinos vs Sanfrecce Hiroshima | 2.20 | 3.25 | 2.95 |
| 04. 06/07/22 | 13:00 | Jubilo Iwata vs Avispa Fukuoka | 2.85 | 2.95 | 2.44 |
| 05. 06/07/22 | 13:00 | Vegalta Sendai vs Ventforet Kofu | 2.28 | 3.10 | 2.95 |
| 06. 06/07/22 | 13:00 | Incheon Utd vs Suwon City | 2.18 | 3.14 | 3.09 |
| 07. 06/07/22 | 13:00 | Suwon Samsung vs Daegu | 2.56 | 3.15 | 2.56 |
| 08. 06/07/22 | 13:00 | Roasso Kumamoto vs Tokushima Vortis | 2.60 | 2.90 | 2.70 |
| 09. 06/07/22 | 13:00 | V Varen Nagasaki vs Montedio Yamagata | 2.21 | 3.09 | 3.09 |
| 10. 06/07/22 | 13:00 | Jeonnam Dragons vs Gyeongnam | 2.70 | 3.10 | 2.46 |
| 11. 06/07/22 | 13:30 | FC Seoul vs Jeonbuk Hyundai | 3.09 | 3.14 | 2.19 |
| 12. 07/07/22 | 19:00 | Grorud IL vs Sandnes Ulf | 2.60 | 3.34 | 2.40 |
| 13. 07/07/22 | 19:00 | Kristiansund vs Tromso | 2.80 | 3.45 | 2.33 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BAYERN MUNICH WAJITOSA KWA DE LIGT

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich inataka kumsajili beki wa kati wa Juventus, Matthijs de Ligt, 90min imethibitisha.


Mholanzi huyo ameingia katika miaka yake miwili ya mwisho ya mkataba wake na mazungumzo ya kuongeza muda wake yamegonga mwamba, huku kukiwa na uwezekano mkubwa wa yeye kuondoka pale kwenye dimba la Allianz.

Chelsea wanamtaka sana De Ligt, huku kocha Thomas Tuchel akimsihi mmiliki Todd Boehly kujaribu kufanya makubaliano, lakini vyanzo vimethibitisha kuwa watalazimika kuzuia ushindani kutoka kwa Bayern ili kumsajili.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga wana mabeki watatu pekee kwenye orodha yao baada ya kuondoka kwa Niklas Sule kwenda Borussia Dortmund majira ya joto, na maafisa wa klabu wamemtambua De Ligt kama mbadala bora wa Mjerumani huyo.

Chelsea wanajikuta katika boti kama hiyo msimu huu wa joto huku wakitafuta kuziba pengo la Antonio Rudiger na Andreas Christensen waliokwenda Real Madrid na Barcelona, na mazungumzo bado yanaendelea na Juve juu ya uwezekano wa kumnunua De Ligt.

Sio Bayern wala Chelsea ambao wako tayari kufikia bei ya Juventus ya euro milioni 100, na sasa klabu zote mbili zinapambana kutoa ofa yao kwa Bianconeri.



## *Dybala akaribia kutua Inter Milan*

**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter Milan inakaribia kumsajili Paulo Dybala licha ya wapinzani wao wa jiji moja, AC Milan wakiwa pia wanamuwania.

Dybala aliondoka Juventus kama mchezaji huru msimu huu wa joto baada ya kushindwa kufikia makubaliano ya mkataba mpya.

Fowadi huyo alikuwa kwenye mazungumzo na Juventus kuhusu kuongeza muda na hata kukubaliana juu ya mkataba mpya wa miaka mitano wenye thamani ya euro milioni 8 kabla ya Krismasi.

Hata hivyo, baada ya masharti hayo kubadilishwa na Juve dakika za mwisho kutokana na rekodi ya fowadi huyo kuwa na majeraha, mazungumzo yalivunjika.

Na sasa Nerazzurri hao wameamua kuingia kwa miguu yote kuwania saini ya Dybala baada ya kuondoka Juve.

Kocha wa Milan, Stefano Pioli ametoa maoni yake kuhusu uvumi unaomzunguka Dybala, na vilevile klabu hiyo inamtaka nyota wa Club Brugge Charles De Ketelaere, akisema: "De Ketelaere na Dybala ni watu wawili tofauti sana. Ninawaacha wasimamizi wafanye maamuzi, watafanya uamuzi bora kwa timu."

798,111/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/07/22 | 22:30 | Criciuma SC vs Vasco da Gama | 2.53 | 2.82 | 3.12 |
| 02. 10/07/22 | 00:30 | Sampaio MA vs Ituano SP | 2.47 | 2.98 | 3.03 |
| 03. 10/07/22 | 02:00 | Charlotte FC vs Nashville | 2.45 | 3.22 | 2.97 |
| 04. 10/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs New York Red Bulls | 2.92 | 3.57 | 2.31 |
| 05. 10/07/22 | 02:30 | Goias vs Atletico Pr | 2.89 | 3.08 | 2.54 |
| 06. 10/07/22 | 03:30 | Houston Dynamo vs Dallas | 2.36 | 3.47 | 2.92 |
| 07. 10/07/22 | 08:00 | Consadole Sapporo vs Kashima Antlers | 2.89 | 3.34 | 2.47 |
| 08. 10/07/22 | 13:00 | Sagan Tosu vs Kashiwa Reysol | 2.32 | 3.23 | 3.23 |
| 09. 10/07/22 | 13:00 | Omiya Ardija vs Tokyo Verdy | 2.71 | 3.32 | 2.56 |
| 10. 10/07/22 | 13:00 | Oita Trinita vs Fagiano Okayama | 2.47 | 3.00 | 3.10 |
| 11. 10/07/22 | 13:00 | Avispa Fukuoka vs Kyoto Sanga | 2.62 | 2.97 | 3.02 |
| 12. 10/07/22 | 13:00 | Suwon City vs FC Seoul | 2.90 | 3.35 | 2.42 |
| 13. 10/07/22 | 16:00 | Utsiktens BK vs Osters IF | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 14. 10/07/22 | 16:00 | Seinajoen JK vs Honka | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 15. 10/07/22 | 19:00 | Sandefjord vs Aalesunds | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 16. 10/07/22 | 21:00 | CA Platense vs Newell'S Old Boys | 2.62 | 3.07 | 2.92 |
| 17. 10/07/22 | 22:00 | Corinthians vs Flamengo | 2.73 | 3.08 | 2.68 |


MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 06/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 1828 | Logan Lightning vs Brisbane City | 2.66 | 3.74 | 2.19 |
| 13:00 | 1193 | Jubilo Iwata vs Avispa Fukuoka | 3.04 | 2.94 | 2.32 |
| 13:00 | 1304 | Tochigi SC vs Tokyo Verdy | 3.03 | 2.98 | 2.30 |
| 13:00 | 1323 | Kashiwa Reysol vs Nagoya Grampus | 2.40 | 2.95 | 2.90 |
| 13:00 | 1479 | Roasso Kumamoto vs Tokushima Vortis | 2.45 | 2.94 | 2.84 |
| 13:00 | 1778 | Renofa Yamaguchi vs Oita Trinita | 3.04 | 3.04 | 2.26 |
| 13:00 | 2446 | Kawasaki Frontale vs Sagan Tosu | 1.67 | 3.53 | 4.61 |
| 13:00 | 2567 | Incheon Utd vs Suwon City | 2.43 | 3.14 | 2.70 |
| 13:00 | 2828 | Jeonnam Dragons vs Gyeongnam | 2.47 | 3.21 | 2.61 |
| 13:00 | 3396 | V Varen Nagasaki vs Montedio Yamagata | 2.18 | 3.09 | 3.14 |
| 13:00 | 3872 | Vegalta Sendai vs Ventforet Kofu | 2.40 | 3.19 | 2.70 |
| 13:00 | 3950 | Yokohama F Marinos vs Sanfrecce Hiroshima | 2.24 | 3.30 | 2.86 |
| 13:00 | 4335 | Kashima Antlers vs Cerezo Osaka | 1.89 | 3.44 | 3.59 |
| 13:00 | 4487 | Suwon Samsung vs Daegu | 2.55 | 3.09 | 2.60 |
| 13:00 | 4570 | Shonan Bellmare vs Gamba Osaka | 2.05 | 3.08 | 3.47 |
| 13:00 | 4655 | Niigata Albirex vs JEF United Chiba | 1.98 | 3.09 | 3.68 |
| 13:00 | 4796 | Yokohama vs Blaublitz Akita | 1.64 | 3.49 | 4.91 |
| 13:00 | 4849 | Machida Zelvia vs Mito Hollyhock | 2.09 | 3.05 | 3.39 |
| 13:00 | 5010 | Fagiano Okayama vs Omiya Ardija | 1.96 | 3.04 | 3.83 |
| 13:00 | 5178 | Vissel Kobe vs Shimizu S Pulse | 1.86 | 3.39 | 3.74 |
| 13:00 | 5610 | FC Tokyo vs Consadole Sapporo | 2.12 | 3.34 | 3.04 |
| 13:00 | 5806 | Zwiegen Kanazawa vs Thespakusatsu | 2.06 | 3.09 | 3.43 |
| 13:30 | 1282 | Busan I Park vs Gimpo Citizen | 2.16 | 3.35 | 2.96 |
| 13:30 | 1305 | Anyang vs Chungnam Asan | 2.20 | 3.28 | 2.94 |
| 13:30 | 4841 | Urawa Red Diamonds vs Kyoto Sanga | 1.60 | 3.52 | 5.28 |
| 13:30 | 4862 | Hangzhou NG vs Dalian Aerbing | 1.87 | 3.25 | 3.89 |
| 13:30 | 5185 | FC Seoul vs Jeonbuk Hyundai | 3.10 | 3.10 | 2.20 |
| 13:30 | 5757 | Eastern Suburbs vs Moreton Bay Utd | 2.33 | 3.79 | 2.46 |
| 15:00 | 5046 | FM Auska Alytaus vs FA Siauliai B | 1.54 | 4.21 | 4.70 |
| 16:00 | 4443 | Mtibwa Sugar vs Tanzania Prisons | 2.09 | 2.80 | 4.10 |
| 16:00 | 4965 | Riteriai B vs FK Babrungas Plunge | 2.60 | 3.59 | 2.29 |
| 17:00 | 3495 | Tobol Kostanay vs Ferencvaros TC | 3.59 | 3.54 | 1.93 |
| 18:00 | 2579 | FK Auda vs BFC Daugavpils | 1.61 | 3.88 | 4.52 |
| 18:30 | 1925 | EIF Ekenas vs IF Gnistan | 1.78 | 3.88 | 3.58 |
| 18:30 | 2517 | FF Jaro vs Pepo Lappeenranta | 1.54 | 4.03 | 4.91 |
| 18:30 | 2840 | PK-35 vs Kerho 07 | 2.08 | 3.58 | 2.94 |
| 18:30 | 3086 | KPV Kokkola vs Japs | 1.70 | 3.62 | 4.21 |
| 18:30 | 4707 | MP Mikkeli vs Pif Jalkapallo | 1.49 | 4.13 | 5.31 |
| 18:30 | 5842 | Lahden Reipas vs Peka | 1.21 | 6.10 | 9.06 |
| 19:00 | 1215 | FK Banga B vs FK Minija | 2.06 | 3.28 | 3.23 |
| 19:00 | 1733 | FK Vilnus Bfa vs Vmfd Zalgiris-3 | 3.25 | 3.70 | 2.00 |
| 19:00 | 1858 | Kedainiai Nevezis vs FK Garliava | 1.30 | 5.10 | 7.26 |
| 19:00 | 4991 | HJK Helsinki vs Rigas Futbola Skola | 1.78 | 3.65 | 4.10 |
| 19:00 | 5375 | Bodo Glimt vs KI Klaksvik | 1.09 | 8.03 | 24.09 |
| 20:00 | 4718 | Molde vs Jerv | 1.18 | 7.04 | 12.07 |
| 20:30 | 1393 | Dudelange vs KF Tirana | 2.44 | 3.25 | 2.75 |
| 21:00 | 1610 | Zrinjski Mostar vs Sheriff Tiraspol | 3.29 | 3.24 | 2.14 |
| 21:15 | 2768 | Maribor vs Shakhter Soligorsk | 1.75 | 3.45 | 4.59 |
| 21:30 | 2581 | Slovan Bratislava vs Dinamo Batumi | 1.58 | 3.91 | 5.21 |
| 22:00 | 2232 | England W vs Austria W | 1.15 | 6.46 | 12.72 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# ZFF KUONGEZA MUDA WA KUPOKEA MAONI

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya Mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar, ZFF, imeendelea kupokea maoni ya kanuni kuelekea msimu mpya wa ligi wa mwaka 2022-2023.

Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti wa kamati hiyo Ali Bakari 'Cheupe' alisema Kamati hiyo ilitoa siku 10 kwa klabu na wadau wa mpira kutoa maoni hayo kwa kanuni mpya.

**Alisema kuwa kwa upande wa klabu kamati hiyo imepokea maoni ya moja kwa moja kutoka Bodi ya Ligi kwa Unguja na Pemba.**

Alisema kuwa kanuni ya msimu huu itaendelea kuwa bora kama ilivyo ya msimu uliopita na kufanyia maboresho zaidi changamoto zilizijitokeza kwa msimu uliopita.

"Tunaendelea na zoezi la kupokea maoni kwa klabu na wadau wa mpira wa miguu Zanzibar, mwamko umekuwa mzuri zaidi kwa klabu zote," alisema.

Aidha alisema kuwa mwisho wa kupokea maoni yao ilikuwa ni jana, lakini Kamati hiyo itaangalia kama kutakuwa na uwezekano wa kuongeza muda wa kuendelea kupokea maoni.

Alisema kanuni ya mwaka huu itatoka mapema na klabu zitaipata kwa wakati kwa ajili ya kuanza mashindano ya ZFF.



Wananchi wakiangalia mchezo wa kichina katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simba Queen yazidi kushusha majembe*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeendelea kusajili wachezaji wa mpira wa miguu kwa timu ya soka ya wanawake, baada ya jana kumtambulisha straika hatari raia wa Ghana, Philomena Abakar kutoka Berry Ladies.

Kupitia akaunti yao ya instagram, Simba Queens ilimtambulisha mchezaji huyo, ikimkaribisha kwa maandishi yafuatayo

"Tumekamilisha usajili wa mshambuliaji Philomena Abakah kutoka Berry Ladies inayoshiriki Ligi Kuu nchini Ghana. Karibu unyamani."

Klabu ya Berry Ladies ya Ghana nayo ilimuaga straika wao tegemeo kwenye mtandao wao wa kijamii wa 'twitter', ikimtakia kila la kheri kwa mchango wake mkubwa ulioiwezesha klabu yao kuwa mabingwa wa msimu hivi karibuni.

Simba Queens kwa sasa ipo kwenye maboresho ya timu hiyo, kabla ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo yanaanzia kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Michuano hiyo inatarajiwa kufanyika nchini msimu huu.

Tayari timu hiyo imemtambulisha straika mwingine raia wa Nigeria Ibinabo Alex kutoka klabu ya Confiuennce Queens ya nchini humo.

Kabla ya hapo, ilimshusha kiungo mkabaji kutoka nchini Kenya, Aquino Corazone kutoka Gaspo Youth.

Kiungo huyo alikuwa na kikosi cha Harambe Starlet mwaka 2019 nchini kilichotwaa Kombe la CECAFA kwa kuifunga Twiga Stars mabao 2-0, fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Zipo taarifa pia, huenda ikamsajili Mganda, Topista Situma kutoka Vihiga Queens, baada ya mchezaji huyo kuvunja mkataba wa klabu yake kwa makubaliano maalum.

# Michezo

Jumatano Julai 6, 2022

Nipashe




Man U yapambana kumbakiza Ronaldo

UKURASA 21



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, Katibu wa Wizara hiyo, Dk. Hassan Abbasi na Rais wa Shirikisho la Mpira wa miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia pamoja na wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake wenye umri chini ya miaka 17 (Serengeti Gils) kabla ya hafla ya kuwapongeza iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Manara amwangukia rais TFF, ataka adhabu

**Na Saada Akida**

MSEMAJI wa Yanga, Haji Manara amemwomba radhi Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia kutokana na tukio lililotokea Arusha kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid wakati wa mechi ya Fainali ya Kombe la Shirikisho, FA, kati ya Yanga na Coastal Union.

**Baada ya tukio hilo, Manara alifunguliwa shauri mbele ya kamati ya maadili iliyochini ya TFF kutokana na kile ambacho kilichotokea Jumamosi kwenye mchezo huo.**

Awali ilionekana video fupi iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii kutokea Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, ikimwonesha ofisa huyo wa Yanga ni kama akitupiana maneno na Rais wa TFF, Karia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Manara alisema: "Nimekutana Karia na kumwomba msamaha kwa kitendo ambacho kimejitokeza siku ya fainali Arusha, kama muungwana nimejua makosa yangu na namwomba radhi rais wa TFF.

"Nilikosea kujibizana na rais wa TFF, Karia, ninaomba radhi, lakini haimaanishi nisiadhibiwe.

"Juzi nilienda kwake kumuomba msamaha tulikunywa, kufurahi na kupiga picha, najua kama binadamu ukilinganisha na tensheni ya mechi ilivyokuwa nilijikuta namjibu japo sikumjibu vibaya wala tusi lolote."

Wakati huo huo, wakati heka heka za uchaguzi wa Yanga zikiwa zimepamba moto, mgombea wa urais, Hersi Said na makamu, ameainisha mambo matano atakayoyapa kipaumbele akichaguliwa kuiongoza.

## Injia Hersi aainisha mambo matano akishinda kuwa rais wa Yanga kwa...

Uchaguzi wa Yanga unatarajiwa kufanyika Jumamosi hii katika ukumbi wa kimataifa wa Julias Nyerere, Dar es Salaam kwa klabu hiyo kupata viongozi wapya baada ya walioko sasa kumaliza muda wao.

"Nimekuwa mgombea pekee basi nisingeweza kueleza chochote, nimegombea nafasi hii ili kuitoa klabu hiyo hapa ilipo kufika mbali zaidi na Wanayanga wanapotarajia kuona timu yao kuwa mbali," alisema.

"Kama nitapata dhamana ya kuwa Rais kuna mambo matano nitayafanya kushirikiana na viongozi wenzangu, ni klabu kongwe tunajivunia ukongwe, lakini ni aibu kutokuwa na miundombinu bora.

Alisema katika miundombinu hiyo atahakikisha unajengwa uwanja katika eneo lao la Kaunda ambao unaweza kuchukua mashabiki 20,000 na pia wataendesha soka kisasa.

"Nitaenda kusimamia mabadiliko yote kwa mujibu wa katiba yetu, nakwenda kuweka mahusiano mazuri na wanachama na klabu yao na eneo hilo tayari tumeshafanya na tayari tumeanza kupata matawi zaidi ya 700. Nikipata nafasi ya kuwa kiongozi tunaenda katika hatua ya pili kupata mashabiki."

Pia alisema ataimarisha uchumi wa klabu, kuushinda mataji, kujenga uimara wa timu za vijana na kuweka jitihada kwenye timu ya wanawake ya Yanga Princess.

Jambo la mwisho ni kuhakikisha wanajenga ushirikiano kati ya klabu na wanachama, mashabiki na wadau wote wa soka ikiwamo kuleta mahusiano mazuri kwa Taifa kuhakikisha wanajenga maendeleo ya michezo nchini.

# Samia akunwa na Serengeti Girls

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu amesema kwake jana ilikuwa ni siku nyingine ya furaha sana sio kwake binafsi tu bali kwa taifa zima, wakati akiipongeza timu ya taifa ya wasichana chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Girls, katika hafla iliyofanyika Ikulu Dar es Salaam.

Rais Samia alisema kuwa anaipongeza Sengereti Girls kwa kufuzu kucheza kombe la Dunia Oktoba mwaka huu nchini India, katika hafla iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam jana.

Alisema hiyo ni rekodi mpya ambayo haijapata kutokea kwa miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania kwa timu ya soka kufuzu kombe la Dunia.

"Nitoe pongezi kwa viongozi wenu waliosimamia mechi na benchi zima la ufundi. Leo (jana) Taifa linajivunia, haikuwa rahisi," alisema Samia.

Aliongeza: "Ushindi wenu umekuwa wa kujivunia sana pale mlipowatandika Cameroon, nchi yenye sifa zote za mpira wa miguu kwa wanawake na wanaume. Lakini Mungu alisimama nasi mkawapa matano yao na sisi wakatupatia zawadi ya moja wakasepa.

"Lakini timu hii imefuzu kushiriki Kombe la Dunia si tu kwa mpira wa miguu wa Wanawake hapa Tanzania, bali hata kwa Wanaume hawajawahi kushiriki Kombe la Dunia la Mpira wa Miguu.

"Nafahamu juhudi zenu zilipelekea kuzifunga timu kama Burundi (5-2), Botswana (11) kila mmoja mlimpa goli lake. Na Cameroon pamoja na visa vyao mliwaachia 5 zao. Kwakweli mmeliweka Taifa mahali pazuri.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >